

HADITHI FUPI ZA KISASA ZA KISWAHILI

KAMA UTANZU MAHULUTI.

NA

LILIAN MAKONJIO MUKOPI

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenya.

Aprili, 2005

Mukopi, Lilian
*Hadithi fupi za
kisasa za Kiswahili.*



05/277412

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY
KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine.

Sahihi: 

LILIAN . M. MUKOPI

Tarehe: 27/06/05

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu.

Sahihi: 

DKT. R.M. WAFULA

Tarehe: 27/06/2005

Sahihi: 

BW. P.J.M. MUGAMBI

Tarehe: 27/06/2005

TABARUKU

Naitabarukia kazi hii kwa marchemu Baba yangu Justus Mukopi, Mamangu mpendwa Beatrice Mukopi pamoja na dada zangu Jessy, Laura, Beril na ndugu yangu Coitydo. Mwisho, naitabarukia kazi hii pia kwa rafiki yangu wa karibu Amwayi Javan kwa moyo alionipa, ili kuikamilisha kazi hii.

1.3 Madhamuni ya utafiti

1.4 Naitabarukia kazi hii

1.5 Sababu za kuchagua mada

1.6 Mipaka ya utafiti

1.7 Mifano ya utafiti

1.8 Mifano za kutambua data

1.9 Mifano za kutambua data

SURA YA FILI

2.1 Mipaka

2.2 Mifano ya utafiti

2.3 Mifano ya utafiti

2.4 Mifano ya utafiti

2.5 Mifano ya utafiti

2.6 Mifano ya utafiti

2.7 Mifano ya utafiti

2.8 Mifano ya utafiti

2.9 Mifano ya utafiti

YALIYOMO

	<u>Page</u>
Ungamo-----	ii
Tabaruku-----	iii
Yaliyomo -----	iv
Shukrani -----	v
Ikisiri -----	v
Ufafanuzi wa Istilahi -----	vi
SURA YA KWANZA	viii
1.1 Utangulizi-----	1
1.2 Swala la Utafiti-----	2
1.3 Madhumuni ya utafiti-----	3
1.4 Nadharia tete za utafiti-----	4
1.5 Sababu za kuchagua mada-----	4
1.6 Upeo na mipaka ya utafiti-----	6
1.7 Misingi ya nadharia-----	7
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii-----	12
1.9 Mbinu za utafiti-----	18
1.10 Mbinu za ukusanyaji data-----	19
1.11 Mbinu za kuchanganua data-----	19
SURA YA TANO	
SURA YA PILI	
2.0 Utangulizi-----	20
2.1 Historia-----	20
2.2 Usimulizi na uandishi-----	30
2.2.1 Kuongezca-----	31
2.2.2 Uziada au yasiyohitajika-----	33
2.2.3 Umbo-----	34
2.2.4 Matumizi ya methali-----	35
2.2.5 Kukaribia maisha ya binadamu-----	36
2.2.6 Nyimbo-----	38
2.2.7 Kutokamilika-----	39
2.3 Hitimisho-----	40

SURA YA TATU

3.0 Utangulizi-----	42
3.1 Mazungumzo-----	42
3.2 Methali-----	58
3.3 Kutokamilika -----	65
3.4 Nyimbo-----	65
3.5 Uradidi-----	67
3.6 Monolojia au uzungumzi nafsia-----	69
3.7 Kuchanganya ndimi-----	72
3.8 Hitimisho-----	74

SURA YA NNE

4.0 Utangulizi-----	76
4.1 Maelezo katika aya -----	78
4.2 Matumizi ya barua-----	88
4.3 Upenyezi wa mwandishi-----	91
4.4 Hitimisho-----	93

SURA YA TANO

5.0 Utangulizi-----	95
5.1 Hitimisho na matokeo ya utafiti-----	95
5.2 Mchango-----	100
5.3 Mapendekezo-----	101
Marejeleo-----	103

SHUKRANI

Natoa shukrani zangu kwanza kwa mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu za kuifanya kazi hii. Shukrani zangu pia ziwaendee wasimamizi wangu walionisaidia kwa chochote nilichohitaji kufanikisha kazi hii. Mwalimu Mugambi aliniongoza popote pale, na pia Dkt Wafula alinipa mawaidha na kunitia moyo. Natoa shukrani zangu kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa mwongozo na mawaidha yao. Ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu walionihimiza kuendelea na kazi hii hadi mwisho hasa Njeri , Babusa, Mary na Savala miongoni mwa wengine.

Nawashukuru wazazi wangu walionisaidia kwa kila hali, ndugu na dada zangu walionihimiza ili kufikia lengo langu. Namshukuru mjomba Nelson Wawire na namshukuru Amwayi kwa kunihimiza kila wakati nilipojihisi siwezi kuendelea. Mwisho namshukuru Joyce Mudolla aliyenichapia kazi hii.

IKISIRI

Katika tasnifu hii tumechunguza umahuluti katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Tumetumia vitabu vitatu vya vya hadithi fupi za Kiswahili za hivi karibuni. Vitabu hivyo ni *Pendo la Heba* (1997), *Mwendawazimu Na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi Na Hadithi Nyingine* (2004).

Malengo ya tasnifu hii yalikuwa kuchunguza umahuluti katika hadithi fupi za Kiswahili. Tumelenga kuchunguza jinsi sifa za usimulizi zinavyoingiliana na sifa za uandishi katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Kutokana na utafiti huu tumepinga madai ya hapo awali kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni zao la ngano. Tumechukua mtazamo tofauti kuwa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili ni mwingiliano wa sifa za usimulizi na uandishi na siyo mwendelezo wa kistari wa ngano. Kulingana na utafiti huu iliibuka kuwa umahuluti huu unajitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Sifa za usimulizi na za uandishi zinajitokeza, huku zikichangiana ili kuzua utanzu huu wa hadithi fupi.

Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi imeshughulikia swala la utafiti, sababu za kuchagua mada, madhumuni ya utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada hii na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili, tumejadili sifa za usimulizi na pia sifa za uandishi kwa jumla. Sifa hizi ziliwekwa wazi na tofauti pia kati ya uandishi na usimulizi zikabainishwa. Tumecangazia sifa kama kuongezea, uziada, matumizi ya vitendawili na methali, kukaribia maisha ya binadamu, nyimbo na kutokamilika kwa mazungumzo. Katika sura ya tatu, tumejadili sifa za usimulizi. Tumejadili sifa hizi za usimulizi na jinsi zinavyorutubisha uandishi. Tumecangazia sifa kama mazungumzo, monolojia, matumizi ya methali, nyimbo, kutotiririka kwa mazungumzo, uradidi na kuchanganya ndimi.

Tumetoa mifano ya matumizi ya sifa hizi kutoka kwa vitabu vitatu. Hivi ni *Pendo La Heba* (1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Katika sura ya nne tumecangazia sifa za uandishi. Tumetazama sifa kama matumizi ya aya, matumizi ya barua na mwisho matumizi ya upenyezi wa mwandishi.

Sura ya tano ambayo ni ya mwisho ni hitimisho na matokeo ya utafiti kwa jumla. Inashugulikia pia mapendekezo ya utafiti ambayo ni kutafiti zaidi kuhusu umahuluti katika hadithi fupi ya kisasaa.

UFAFANUZI WA ISTILAHU

Istilahi hizi zitatumika kuzingatia maana zifwatazo:

- Changamano - Ni kutumika pamoja
- Kisaasili - Kisa cha mianzo ya matendo yaliyozoelewa kama unyago, tohara na imani mbalimbali
- Kisakale - Kisa cha kale kinachohusu matukio ya kweli kihistoria juu ya kikundi cha watu.
- Kistari - Mwendeleo wa mtiririko; moja kwa moja
- Mahuluti - hali ya utamaduni, utanzu au sifa za Kibinadamu zinazotokana na vitu tofauti kuzingatia utafiti huu umahuluti ungashiria mwingiliano wa uandishi na usimulizi.
- Matini - Kazi iliyoandikwa au iliyotamkwa
- Mwingiliano matini - Dhana inayoeleza kupiga mwangwi katika matini nyinginezo. Matini hizi huwa zilizotangulia, zilizopo na zitakazojiri baadaye.
- Nadharia ya - Nadharia inaelezea kubadilika kwa viumbe, ubadilikaji vitu na utamaduni kutoka kwa kiwango cha chini hadi cha juu. Kwa mujibu wa kazi hii ni ubadilikaji wa utamaduni wa usimulizi hadi uandishi.
- Ngano - Hadithi za paukwa pakawa na wakaishi raha Mstarehe. Masimulizi ya matukio yenye husemwa na huzingatia maadili katika jamii.

- Tarihi** - Masimulizi yanayowasilisha kimapokeo visa, ukweli fulani wa kihistoria juu ya kikundi fulani cha jamii. Visa vinayosimuliwa ni kama njaa na vita na magonjwa.
- Uandishi** - Jinsi ya kuhifadhi habari ndefu au fupi katika maandishi.
- Usemizano** - Ni usemi ujidhihirishao baina ya sauti mbili. Mtagusano unaohusu kuingiliana kwa sauti mbili katika majibizano.
- Usimulizi** - Kuwasilisha kwa njia ya mdomo

SURA YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Hadithi fupi ya kisasa ni utanzu ambao ni mchanga na haujashughulikiwa na wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili. Utanzu huu umeanza hivi karibuni na kuchapishwa katika miaka ya sabini. Utanzu huu umekuwa sana na hasa kiuchapishaji katika fasihi za lugha zingine za Ulaya ikilinganishwa na Kiswahili (Wamitila 2002:66). Lakini hilo silo swala la kushangaza ikimbukwa kuwa fasihi ya Kiswahili bado inakua.

Baadhi ya machapisho katika utanzu huu ni kama vile: *Parapanda na Hadithi nyingine* (1974) na *Uwike Usiwike Kutakucha* (1978) vya Ruhumbika, *Kicheko cha Ushindi* (1978) cha M.S. Mohamed, *Dhuluma na hadithi nyingine* (1980) cha Barshad, *Tamaa Mbele na Hadithi Nyingine* (1980) na *Nipe Nikupe na Hadithi Nyingine* (1982) vya Banzi, *Twen'zetu Ulaya na Hadithi nyingine* (1984) cha Macha, *Jamila Mpenzi na Hadithi Nyingine* (1989) cha Senkoro, *Nitakuja kwa siri* (1981) cha Msokile, *Pendo la Heba* (1997) kilichohaririwa na Wafula na King'ei, *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) kilichohaririwa na Mbatiah na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) kilichohaririwa na Wamitila.

Hadithi fupi ya kisasa katika Kiswahili ni sehemu ya maendeleo ya jamii. Licha kwamba kwa sababu ya uchanga wake haijashughulikiwa

sana, Mohochi (2000) anasema utanzu huu umedharauliwa lakini una maana kwa kizazi cha sasa na hata cha baadaye, kama tanzu zingine kama Tamthilia na Riwaya.

Pamoja na kwamba hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili imezaliwa hivi juzi, inapaswa kushughulikiwa kitaaluma. Tanzu zingine za fasihi, hasa fasihi simulizi kama vile visasili, visakale na tarihi, zinashabihi hadithi fupi ya Kiswahili.

Kushabihiana huku kunasababishwa na ufupi wa tanzu hizi na kutumia lugha ya kinathari. Jambo hili limewaelekeza baadhi ya wahakiki kufikiri kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni kimelea cha tanzu za fasihi simulizi. Tanzu hizi kama ilivyotajwa hapo juu ni kama ngano, tarihi, visasili na visakale. Utafiti huu una madai tofauti na yale ya kuelezea sifa za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili kistari. Kinyume na hayo, tumconyesha kwamba utanzu unasawiri sifa mahuluti.

1.2 SWALA LA UTAFITI

Wahakiki wa hapo awali kama vile Msokile (1988), Sengo (1988) Senkoro (1987), Msokile (1992), Mohochi (1995) wamekuwa na maoni kuwa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili ni kimelea cha ngano ya kale. Madai yao ni kuwa ngano hizi zimeendelea kistari hadi zikawa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Tofauti na maoni yao utafiti huu

umeshughulikia utanzu huu wa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili kama utanzu mahuluti. Utafiti huu umconyesha kwamba sifa za usimulizi na uandishi sifa zinatokea sambamba katika hadithi fupi za kisasa katika fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu ulijishughulisha na kuonyesha umahuluti unavyojitokeza katika hadithi fupi. Umahuluti huu unazingatia sifa za usimulizi na sifa za uandishi, na jinsi zilivyoingiliana ili kuibua hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Utafiti wetu umcongozwa na maswala yafuatayo:-

- (i) Je utanzu huu una sifa za usimulizi?
- (ii) Sifa hizi ni zipi?
- (iii) Utanzu huu umedhihirisha sifa za uandishi?
- (iv) Sifa hizi ni zipi?
- (v) Je sifa hizi zimehusiana vipi, ili kuunda umahuluti katika hadithi fupi?

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu yamekuwa :

- 1) Kulirejelea swala la sifa za hadithi fupi
- 2) Kuonyesha jinsi mbinu zinazotokana na fasihi simulizi na uandishi zinavyodhihirika katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.
- 3) Kudhihirisha kuwa hali ya umahuluti ndiyo hali halisi ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

1.4 NADHARIA TETE

1. Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili hazijazalishwa kistari kutoka kwa ngano.
2. Hadithi fupi za kisasa za Kiswahili zina sifa zinazotokana na utaalamu wa uandishi na sifa zinazotokana na utaalamu wa usimulizi. Sifa hizi zinatokea sambamba katika mtiririko wake.

1.5 SABABU ZA KUCHANGUA MADA HII

Swala la sifa za hadithi fupi limekuwa muhimu kwa wataalamu wengi wa hadithi fupi. Wamitila (2002:67) anamnukuu Poe, akipitia kitabu cha *Tales cha Nathaniel Hawthorne* alisema hivi:

Hadithi fupi si sura katika riwaya, wala tukio ambalo limechopolewa katika hadithi fupi au kisa kirefu, bali humvutia na kumteka msomaji na kumfanya aamini kuwa ingeweza kuharibika ikiwa itakuzwa na kuwa ndefu au kama itafanywa sehemu ya kazi kubwa.

Kutokana na maelezo haya, sifa za hadithi fupi kama utanzu unaojitegemea na wa kipekee zinajitokeza. Hata hivyo swala hili la sifa za hadithi fupi bado linafaa kurejelewa upya tukirejelea maoni ya mwanzilishi wa utanzu huu kuendelea hadi sasa. Kwa sababu ya maoni mengi kuhusu sifa za hadithi fupi za kisasa, inafaa kutazama upya sifa, za hadithi fupi.

Utafiti huu pia umedhamiria kutilia shaka nadharia ya ubadilikaji, ambayo imedunisha tamaduni zenye usimulizi kuwa duni na za nyuma. Nadharia hii imetukuza mataifa ya kimagharibi kuhusu nyenzo za uandishi na kudai kwamba mataifa hayo yameendelea kuliko yale ya utamaduni wa usimulizi. Pana umuhimu wa kuangalia upya madai haya kwa kuzingatia umuhimu wa tamaduni hizi mbili na jinsi zitakavyoingiana.

Ugeni na upya wake umesababisha uhakiki wake na utafiti wake kuwa mchache. Mohochi (2000) anaelezea kuwa tumekosea sana utanzu huu katika misingi hii ya utafiti wa uhakiki. Kwa sababu ya tafiti chache na hakiki chache, katika uwanja wa hadithi fupi hivyo basi ikawa sababu nyingine ya kushughulikia utanzu huu ili kuendeleza utafiti wa hapo awali. Kuendeleza utafiti huu ni kuipa hadhi hadithi fupi sawa na hadhi iliyopewa riwaya, tamthilia na ushairi katika fasihi ya Kiswahili.

Uandishi wa mwanzo wa waandishi wa tanzu zingine za fasihi ulikuwa wa hadithi fupi, baadaye hawaendelezi kipawa hiki cha kuandika hadithi fupi. Makisio ya mtafiti ni kwamba pengine walitumia hadithi fupi kama hatua ya kuwawezesha kujitoma katika ubunifu wa kisanaa kwa upande wa tamthilia na riwaya. Waandishi hawa ni kama Kezilahabi E., Msokile na hata Senkoro. Waandishi hawa walchukulia uandishi wa hadithi fupi kama hatua yao ya

kwanza ya uandishi na hivyo baadaye waliacha kuandika hadithi fupi. Utafiti huu ulichaguliwa ili kuliweka wazi wazo kuwa hadithi fupi ni utanzu wa kipekee unaohitaji ujuzi wake wa kipekee na siyo hatua ya kuanza uandishi katika uwanja wa fasihi.

1.6 UPEO WA UTAFITI

Kuna vitabu vingi vilivyochapishwa katika uwanja wa hadithi fupi za Kiswahili. Miongoni mwa vitabu hivi ni *Parapanda na Hadithi Nyingine*(1974) na *Uwike Usiwike Kutakucha* (1978) vya Ruhambika, *Dhuluma na Hadithi Nyingine* (1980) cha Barshad, *Nipe Nikupe na Hadithi Nyingine* (1982) na *Twen' zetu Ulaya na Hadithi nyingine* (1984) vya Banzi, *Si Wazimu Si Shetani* (1978) cha Mohamed, *Pendo la Heba* (1997) kilichohaririwa na Wafula na King'ei, *Kicheko cha Ushindi*(1978) cha S.A. Mohamed, *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) kilichohaririwa na Mbatiah na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) kilichohaririwa na Wamitila. Hata hivyo miongoni mwa machapisho haya, nimezingatia hadithi zilizoteuliwa katika machapisho matatu. Hayo ni;

- a) *Pendo La Heba* (1997) kilichohaririwa na King'ei na Wafula.
- b) *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) kilichohaririwa na Mbatiah.
- (c) *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) kilichohaririwa na Wamitila.

Sababu za kuchagua vitabu hivi vya hadithi fupi ni:

- a) Kutokana na mapitio ya mwanzo, nilitambua baadhi ya sifa za hadithi fupi. Kutoka na machapisho haya, tumeweza kujibu baadhi ya maswali ya utafiti.
- b) Hadithi hizi zimechapishwa hivi karibuni. *Pendo la Heba* (1997), *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Zingine* (2004) ni hadithi zilizochapishwa michache iliyopita. Vitabu hivi vilituwezesha kufafanua iwapo maendeleo ya Hadithi fupi ni ya kistari au si ya kistari.

Katika vitabu hivi tulishughulikia hadithi tatu kutoka kwa kila kitabu ili kujibu swala la utafiti. Hadithi tatu zilichaguliwa kutoka kwa kila kitabu, ili kuweza kuonyesha sifa hizi na kupeana data ya kutosha kutoka kwa kila kitabu.

1.7 MISINGI YA NADHARIA

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ya mwingiliano matini. Nadharia hii inamaanisha kuingiliana kwa matini, kuchangiana na kutegemeana kwa matini katika kazi moja ya fasihi. Kwa mujibu wa Allen (2000) nadharia hii iliasisiwa na Julia Kristeva. Kristeva alitumia istilahi ya Kiingereza "intertextuality" kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1967. Kristeva (1980) aliyaunganisha mawazo ya Ferdinand De Saussure na ya Bakhtin ili kuibua maana kamili ya

nadharia ya mwingiliano matini. Alisisitiza kuwa katika matini, kuna maana inayozingatia msomaji.

Alirejelea mawazo ya Ferdinand de Saussure akielezea juu ya ishara katika lugha ili kuibua maana. De Saussure alizingatia kuwa katika lugha kuna neno ambalo ni mkusanyiko wa sauti. Katika lugha kuna ishara zinazoashiria kiashiria na kiashiriwa.

Alieleza kuwa hamna ishara katika lugha ambayo ina maana inayojisimamia. Ishara yoyote huwa na maana katika muktadha wa ishara zingine. Allen (2000) katika maelezo yake kuhusu mtazamo wa Ferdinand de Saussure alielezea kuwa ishara huwa na maana, kutokana na uhusiano wake na ishara nyinginezo. Hivyo basi maana zinazojitokeza katika lugha, huwa mara kwa mara za kimuktadha. Maana huzingatia uhusiano na mwingiliano katika mfumo wa lugha.

Hakuna ishara ambayo ina maana asilia. Ishara hutokea katika mfumo wa lugha na hutoa maana katika mahusiano ya ishara zingine katika mfumo mzima unaohusika wa lugha. Mwingiliano wa ishara hizi ulikuwa msingi wa nadharia ya mwingiliano matini.

Nadharia hii katika karne ya ishirini iliendelezwa kujengwa upya na wananadharia wengine kama Bakhtin ambaye ni mwasisi wa nadharia ya usemezano. Bakhtin (1981) anazingatia kuwa kazi yoyote

ya kifasihi lazima ilitie mkazo muktadha wa kihistoria na kijamii kwani umbo la fasihi, ni chombo katika uhakiki wake wa jamii. Anaeleza kuwa semi hasa ni za kisemezano. Kila usemi ni jibu la usemi mwingine. Bakhtin (1986) anaelezea kuwa neno lina pande mbili katika kitendo cha usemaji. Kila neno humlenga msemzwa na msemza.

Lugha yoyote ya usemezano ni ile yenye kuingiliana na isiyokuwa na mwelekeo mmoja, bali mielekeo miwili au zaidi. Nadharia ya usemezano ina uhusiano mkubwa na nadharia ya mwingiliano matini. Nadharia hii inazingatia mwingiliano wa semi na kujibizana katika matini.

Bakhtin (1981) anasema kwamba usemi wa sasa unatokea kwa vile unaathiriwa na usemi wa awali. Usemi wa sasa unatokana na usemi wa hapo awali, na utaathiri ule utakaosemwa hapo baadaye. Semi hizi huathiriana na kuingiliana katika matini.

Kule kuingiliana kwa usemi wa awali, wa sasa na hata wa baadaye ndiyo uliokuwa msingi wa mawazo ya Kristeva katika kuakisi na kuiweka wazi nadharia hii ya mwingiliano matini.

Dhana ya mwingiliano matini iliendelezwa na kikundi cha wanamuundo kama Roland Barthes, katika harakati ya kueleza

matini dhabiti. Roland Barthes akinukuliwa na Allen (2000:13) anasema kuwa;

Matini siyo tu sentensi moja ya maneno inayoibua maana moja tu, bali ni mchanganyiko wa maandishi ambayo siyo ya asili. Matini ni matini nyingi kutoka tamaduni tofauti. Mwandishi ana uwezo wa kuchanganua matini tofauti, na maneno yake huelezwa na maneno mengine (tafsiri yangu).

Hivyo basi Barthes anashikilia kuwa matini hutegemeana, hakuna ambayo hujisimamia. Kwa misingi hii, Kristeva (1980) aliendeleza wazo kuwa kuwepo kwa matini inayotarajiwa kuandikwa au kutamkwa kunasababisha matini iliyopo sasa. Akifafanua zaidi nadharia hii, anaeleza kuwa, mwingiliano matini unazingatia kutegemeana kwa matini mbalimbali katika matini moja ili kuwezesha na kufanya mawasiliano yaliyosemwa au yaliyoandikwa kufaulu. Hivyo basi nadharia hizi mbili zinaingiliana na kufanana kwa kiasi fulani. Hivyo basi tulitumia nadharia ya mwingiliano matini ambayo, ina mawazo sawa na ile ya usemezano.

Wananadharia wa mwingiliano matini wanasema kuwa kuna kusemezana katika matini moja. Nadharia hii inafaa zaidi katika utafiti huu kwa vile umetusaidia kufafanua mwingiliano unaopatikana katika njia za kuwasilisha hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Nadharia hii ilitusaidia kuanisha sifa hizi mbili za usimulizi na uandishi na kuonyesha jinsi zinavyoingiliana ili kuunda utanzu wa hadithi fupi kama utanzu mahuluti.

Kwa mujibu wa Allen(2000), mihimili muhimu iliyotusaidia katika utafiti huu ni:

1. Matini haijitegemei bali huwa ni mwingiliano wa matini nyingi.
2. Mwingiliano wa matini hutokea na kutumiwa katika jamii huku ikizingatia itikadi, mivutano na kukua kwa jamii.
3. Matini ya sasa hutokana na matini ya awali na matini inayotarajiwa kuwepo. Hakuna matini iliyoandikwa bila kuzingatia ile ya awali iliyosemwa au kuandikiwa.
4. Uelewaji wa matini hutofautiana kutoka kwa msomaji mmoja hadi mwingine. Hali hii hutokea kwa sababu ya mwingiliano wa matini ya awali na unaotarajiwa ambao wasomaji tofauti wamepitia.
5. Mwingiliano wa utamaduni itikadi husababisha mwingiliano katika jamii moja au tofauti na hivyo husababisha mwingiliano matini.

Nadharia ya mwingiliano matini imetusaidia kuonyesha mwingiliano kati ya sifa za uandishi na sifa za usimulizi katika hadithi fupi kwa vile inazingatia mwingiliano wa matini.

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Kazi mbalimbali zimeandikwa kuhusu hadithi fupi kwa ujumla.

Sengo (1982) ameshughulikia swala la hadithi fupi kwa ujumla.

Amechanganua utanzu huu na kuonyesha jinsi unavyotofautiana na tanzu zingine za fasihi andishi. Anazungumzia sifa za hadithi fupi kwa ujumla kwa mfano anaeleza aina ya wahusika ambao ni wachache.

Anaelezea kuhusu ploti yake kwa ujumla. Anasema kuwa:

Muundo wa hadithi fupi ni ule wa ngano za hapo awali (77).

Katika kushughulikia hadithi fupi, wazo kwamba hadithi fupi inatokana na ngano linajitokeza wazi. Hata hivyo haelezi kama kuna mwingiliano wa sifa za usimulizi wa ngano na uandishi katika hadithi fupi ya kisasa. Pamoja na haya, wazo hili kwamba hadithi fupi imeanza na kukua kistari kutokana na ngano ndilo linalopingwa katika utafiti huu.

Swala hili pia limeshughulikiwa na Senkoro (1982). Ameshughulikia utanzu huu na kueleza kuwa ulizuka kutoka kwa ngano za hapo awali. Amesema kuwa hadithi fupi ni umbo jipya la ngano za hapo awali. Ameeleza kuwa mandhari ya hadithi fupi huwa ya wazi, na wahusika wachache. Amesisitiza tukio kuu ambalo ndilo nguzo katika hadithi fupi. Utafiti huu utatofautiana na wake kwa vile umezingatia swala la umahuluti na siyo mwendelezo wake

kistari. Kitambo tumesema kwamba utafiti huu unapinga maendeleo ya hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili kistari.

Msokile (1992) naye alieleza hadithi fupi kuwa utanzu unaotumia lugha ya nathari na una wahusika wachache kuliko wale wa riwaya. Pia alizungumzia tukio moja kama mojawapo wa sifa za hadithi fupi. Hata hivyo hakurejelea swala la sifa za usimulizi na uandishi katika hadithi fupi. Utafiti huu umejikita siyo katika kuzungumzia sifa za hadithi fupi kwa ujumla, bali sifa za usimulizi na uandishi na jinsi zinavyotegemeana katika utanzu huu wa hadithi fupi.

Katika tasnifu yake ya uzamili Mohochi (1995) ameeleza kuhusu fani katika hadithi fupi kwa mapana. Ameendeleza kuwa utanzu huu hutumia lugha ya hadithi. Kuna wahusika wachache kuliko wale wa riwaya. Amesisitiza kuwa hadithi fupi ni hadithi tu inayoelezea tukio moja. Ameainisha na kuchanganua ploti pamoja katika utanzu huu. Katika kazi yake, ameelekea kuonyesha kuwa hadithi fupi ni utanzu ambao unatoka kwa ngano za hapo awali zinazoendelea, zikabadilika na kuwa hadithi fupi. Ameelezea kuwa maendeleo haya ni ya moja kwa moja kutoka kwa ngano za hapo awali hadi kufika kwa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.

Katika utangulizi wa *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* (2000) kilichohaririwa na Mbatiah, swala hili la sifa za hadithi fupi

linarejelewa. Mbatiah Anaelezea kwa kifupi maana ya hadithi fupi. Anasema kuwa ni vigumu kufafanua maana yake. Kisha anatoa sifa kuu za hadithi fupi. Sifa hizi anazianisha kama, dhamira moja, mtindo ambao anasema ni matumizi ya lugha kifasaha. Muundo ni jinsi elementi za kazi ya fasihi ziliyoyopangwa ili kujenga kazi nzima. Wahusika wachache na mara kwa mara mmoja hukuzwa. Kando na sifa hizi anasema kuwa:

Hadithi fupi ni masimulizi yaliyoandikwa kwa lugha ya nathari, juu ya tajriba fulani ya maisha... Uti wa mgongo wa hadithi fupi ni hadithi (uk.x).

Hoja ya usimulizi inajitokeza katika ufafanuzi wake. Yeye anashughulikia hadithi fupi kama masimulizi yaliyoandikwa. Tofauti na maoni yake utafiti huu utaonyesha kuwa utanzu huu siyo tu masimulizi yaliyoandikwa bali una maingiliano ya sifa hii ya fasihi simulizi na sifa za uandishi ili kutamba utanzu huu wa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

Wamitila (2002) anatoa historia fupi na jinsi utanzu wa hadithi fupi ulivyoendelea hadi sasa. Anaangazia hadithi fupi kwa kuzingatia sifa ya ufupi, wahusika ambacho anasema ni wachache. Anazungumzia mandhari ya inayobainika wazi. Sawa na wahakiki waliotangulia, anadai kuwa hadithi fupi imeendelea kistari kutoka kwa ngano. Anaeleza kuwa ngano ndicho kiwango cha chini cha hadithi fupi. Utafiti huu umekanusha ule mwendeleo wa kistari, na umeangazia

hadithi fupi kama utanzu ulioibuka kutoka kwa sifa za usimulizi na za uandishi, tofauti na madai yake.

Katika mwongozo wa *The Chameleon's Second Delivery*, (1987) Mwanzi pia anatoa ufafanuzi zaidi wa sifa za hadithi fupi. Katika utangulizi anasema hadithi fupi za kisasa zina mizizi yake katika ngano ambayo husimuliwa kwa dakika ishirini au thelathini. Hadithi fupi huonyesha hali ya mwandishi kuwasilisha wazo lake kwa mda mfupi kwa wasomaji. Hivyo basi anasisitiza kuwa hadithi fupi siyo utanzu ulioibuka kwa kuzuka kwa uandishi bali ni ngano za hapo awali zilizobadilika na kuwekwa katika maandishi. Tukirejelea tasnifu yake ya Uzamifu (1995), anashughulikia mtindo wa hadithi fupi katika hadithi fupi za Ngugi wa Thiong'o, Leonard Kibera na Grace Ogot. Anashughulikia matumizi ya lugha katika hadithi hizi. Analalamika kuwa hadithi fupi ni utanzu uliopuuzwa na waandishi na wahakiki wa fasihi kwa jumla. Anaangaza mazungumzo, taharuki na ishara mbalimbali katika hadithi fupi za waandishi hawa. Anazingatia misingi ya Poe katika kufafanua sifa za hadithi fupi. Anaeleza kuwa Poe anatazama utanzu huu kuwa mfupi. Hadithi fupi yafaa kuwa fupi kuweza kusomwa katika kikao kimoja. Pili, yapaswa kujenga wazo au hisia moja tu kwa kujikita katika mgogoro mmoja; na tatu, tutatuwe mgogoro huo kwa mjengo bora wa ploti. Aidha alisisitiza kuwepo muundo mzuri wa lugha iliyochujwa hivi kwamba, kila neno linachangia katika athari inayotokana na hadithi.

Ufafanuzi wake unatoa mwanga kwa utanzu huu. Mwanzi anaelezea kuwa hadithi fupi ni masimulizi mafupi, yanayoelezea mhusika mmoja. Ploti ya hadithi fupi inahusu matukio yaliyofinyangwa pamoja ili kuzua wazo kuu (uk 11). Anazingatia pia sifa za usimulizi katika hadithi fupi hizi, kwa ujumla na hata za uandishi. Tofauti ya utafiti wake na wetu ni kwamba haunganishi sifa hizi na kuonyesha jinsi zinavyohusisha katika hadithi fupi ili kuzua utanzu mahuluti.

GrandSaigne (1985) katika utangulizi wake, anadai kwamba utanzu huu unaangazwa kama ambao una mizizi yake katika ngano za hapo kale, na hata sasa huendelea kusemwa katika jamii. Ngano huendelezwa hata sasa katika jamii ambazo zina usimulizi, na hata katika maandishi. Anaeleza kuwa baadhi ya hadithi ambazo zimeandikwa zina sifa za usimulizi ambazo zilikuwa katika ngano za awali. Sifa ya fanani au mtambaji na hadhira kama sifa muhimu hadi sasa. Mtambaji huyu ana uhuru wa kutamba hadithi ili jinsi anavyotaka. Anaelezea kuwa katika hadithi fupi hizi zilizoandikiwa, mtambaji huwa mbali sana na hadhira yake.

Anaendelea kuelezea mawazo ya mwanzilishi wa istilahi hii ya hadithi fupi. Anaeleza kuwa Allen Poe ndiye baba wa hadithi fupi. Mnamo mwaka wa (1842) Poe, alieleza sifa za hadithi fupi, kuwa ni utanzu ulio mfupi, ambao unahitaji kusomwa kwa kikao kimoja tu. Jambo

lingine lililosisitizwa na Poe lilikuwa lengo la hadithi fupi ambalo ni kuzua athari moja iliyo ya kipekee. Habari yoyote ambayo haifai kuendelezwa na ambayo haichangii athari hii haifai kuwekwa katika hadithi.

GrandSaigne (1985:2) anaelezea kuwa, kazi nyingi za hadithi fupi huzingatia sifa hizi ambazo zilianishwa na Allan Poe. Zinazingatie mhusika mmoja, tukio moja, hali ambayo ni moja na wakati mmoja. Wengine wanasema siyo lazima hadithi fupi izingatia ule ufupi na umbo mahsusi, bali kuna uhuru. Anatoa mfano wa hadithi ya "Blankets" ya Alex La Guma. Anasema hadithi hii inafaulu kuhusisha mambo ya kale, ya sasa na hata yale matukio ya baadaye. Wazo la hadithi fupi kuwa zao la ngano linajitokeza wazi. Madai yake ni kuwa hadithi fupi ni kimelea cha ngano ya hapo awali.

Wahakiki wa kigeni pia wamezungumzia hadithi fupi hasa katika muktadha wa fasihi ya Kiingereza. Parker (1965:1-88) anashughulikia utanzu huu akiangaza maudhui katika hadithi fupi. Ametoa uchanganuzi wa maudhui pamoja na wahusika wanaojitokeza katika hadithi hizo. Anatoa orodha ya baadhi ya maudhui yanayojitokeza katika hadithi fupi kama vile upole, kifo, njaa, kicheko na upendo. Anashikilia kuwa hadithi fupi nzuri ni ile inayomwelekeza msomaji katika kuyaelewa maisha ya sasa na hata ya baadaye. Parker anashughulikia utanzu huu kama kimelea cha ngano za hapo awali.

Anaeleza kuwa kwa sababu ya mabadiliko katika jamii, ngano za hapo awali ziliendelea kubadilika na kuwa hadithi fupi. Ule mwendeleo ni wa moja kwa moja, tofauti na jinsi utafiti huu ulivyo ushughulikia utanzu huu.

Barley (2000) amechangia kutoa mwangaza kuhusu utanzu huu kwa kushughulikia vijenzi vya hadithi fupi. Anaeleza kuwa wakati katika hadithi fupi ni mfupi sana huku wahusika wakiwa wachache. Anaelezea usimulizi katika hadithi fupi bila kuelezea uandishi au sifa za uandishi.

Kutokana na haya, ni wazi kuwa swala la umahuluti wa hadithi fupi halijashughulikiwa. Wengi wa wahakiki hawa wanashughulikia hadithi fupi kama utanzu ulioendelea kistari hadi sasa kutoka kwa ngano za hapo kale. Utafiti huu hasa umeshughulikia swala la sifa za usimulizi na sifa za uandishi, zinavyotegemeana katika hadithi.

1.8.0 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti wa mada hii ulikuwa wa maktabani. Mtafiti alivisoma vitabu alivyoviteua na kupitia ita tahakiki tofauti, zilizofanywa kuhusu hadithi fupi. Baadaye ametoa muhtasari kuhusu yale aliyoyasoma akizingatia maswala ya utafiti.

1.8.1 MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Vitabu vilivyoteuliwa vimesomwa, na data kuhusu sifa za hadithi fupi ikakusanywa. Makala kuhusu hadithi fupi yalisomwa ili kutusaidia kuelewa sifa za usimulizi na uandishi katika hadithi fupi na jinsi zinavyotumika sambamba katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.

1.8.2 MBINU ZA KUCHANGANUA DATA

Machapisho yaliyoteuliwa yalichanganuliwa kwa mujibu ya nadharia ya mwingiliano matini. Mifano ya sifa za usimulizi na sifa za uandishi, zimebainishwa kuhakikiwa kwa kuzingatia nadharia hii.

Sifa hizi zimezingatiwa kwa pamoja jinsi zinavyotegemeana na kuhusiana ili kuunda utanzu huu wa hadithi fupi. Utafiti huu umeweza kuweka wazi swala la umahuluti katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Mtafiti amewasilisha data yake katika njia ya nathari. Ameyaweka maelezo yake kwa njia ya mtiririko na kuonyesha sifa hizi.

SURA YA PILI

2.0 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita tumezungumzia kuhusu hoja muhimu zinazoshughulikiwa katika tasnifu hii. Hoja hizi ni swala la utafiti madhumuni ya utafiti nadharia tete za utafiti sababu za kuchagua mada hii upco wa utafiti yaliyoandikwa kuhusu mada hii na hatimaye mbinu za utafiti. Katika sura hii lengo letu ni kushughulikia historia ya hadithi fupi katika sehemu ya kwanza. Historia ya hadithi fupi yaonyesha kwamba wahakiki wengi wanafikiria kwamba maendeleo ya utanzu huu wa fasihi ni wa kistari. Katika sehemu ya pili tutazungumzia uhusiano uliopo kati ya uandishi na usimulizi kwa nia ya kuonyesha kuwa nyenzo hizi za mawasiliano zinapotumika hutokea sambamba.

Hadithi fupi kama utanzu mojawapo wa fasihi andishi una hatua zake za maendeleo katika historia yake. Tangu hapo awali wataalamu wamekuwa na mawazo mbalimbali kuhusu chimbuko la utanzu huu na jinsi ambavyo umebadilika na kuendelea hadi sasa.

2.1 HADITHI FUPI: HISTORIA

Hadithi fupi ni utanzu ambao historia yake si ndefu kama tanzu zingine za fasihi. Hata hivyo ni utanzu ambao ni wa maana kama tanzu zingine za fasihi kama ushairi na riwaya.

Mohamed (1995) ana maoni kuwa hadithi fupi ni miongoni mwa tanzu zingine za fasihi kama riwaya, Ushairi na tamthilia. Hizi ni tanzu za kinathari za fasihi ambazo hutokana na masimulizi ambayo daima yamo vichwani mwa wazee. Anawatambua waandishi ambao wameathiriwa na utanzu huu kama Shaaban Robert katika *Kusadikika* (1951) na katika *Siku ya Watenzi Wote* (1968). Anasisitiza kuwa, masimulizi ya hapo zamani ndiyo msingi wa tanzu andishi za Fasihi hivi sasa. Pia anasisitiza kuwa hadithi fupi ni utanzu unaotokana na masimulizi ya hapo kale, yaliyokua hadi sasa na kuwa hadithi fupi.

Mohochi (1997:63) katika makala yake kuhusu "hadithi fupi: utanzu uliodharauliwa" anasema kuwa:

Jamii nyingi zimekuwa na hadithi fupi katika masimulizi ya mdomo na hatimaye katika maandishi Ngano ndiyo aina ya fasihi ambayo ina historia ndefu sana katika jamii.

Mohochi anashikilia kuwa hadithi fupi siyo utanzu ambao ni mgeni, bali historia yake imejengeka katika ngano, ambazo ni za kale sana katika jamii. Anaeleza kuwa hadithi hizi zimekuwa sehemu ya utamaduni wa jamii. Hadithi hizi zilisimuliwa miongoni mwa wavuvi, wawindaji, wanawake nyumbani, katika vyumba vya watoto na hata sasa madarasani, katika viwango mbali mbali. Mohochi anatambua kuwa muda huu wote, binadamu wamesimuliana hadithi fupi kwa minajili ya kuonya kuhusu tabia fulani katika jamii, kuwaburudisha, kuzingatia viwango tofauti vya watu katika jamii na tamasha za sherehe mbali mbali.

Hivi sasa hadithi fupi zinajitokeza siyo katika hali ya ngano, lakini katika miundo na mitindo tofauti. Hivyo basi Mohochi anatilia mkazo kuwa ngano za hapo awali zilitumia mitindo tofauti na hizi za hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Kuibuka kwa maandishi kulizua njia nyingi za kuwasilisha kazi ya sanaa. Hadithi fupi kama mojawapo ya kazi ya sanaa iliathiriwa katika uwasilishaji wake. Mohochi (1997).

Mohochi (1997:4) anasema kuwa baina ya karne ya kumi na tano na kumi na saba, utanzu huu ulipuuzwa na hivyo kudidimia kwa vile wakati huo tenzi na kazi zingine za kitanzia ndizo zilizokuwa kazi muhimu za kinathari miongoni mwa tawala. Lakini ilipofika karne ya kumi na nane na kumi na tisa, hadithi fupi zilianza kuchapishwa magazetini na katika majarida mengi na kuwavutia watu wengi ambao wanapenda kuyasoma magazeti haya. Mohochi anatoa mfano wa Poe (1981) kwa kuitaja hadithi ya the "Two Drivers" ya Walter Scott iliyochapishwa katika *Chronicles of Conongate* (1837) kuwa hadithi ya kwanza ya kisasa katika Kiingereza.

Hivyo basi, hadithi fupi kama utanzu unaojisimamia ulianza kuchapishwa kwenye vitabu na kuwafikia wasomi wengi katika jamii. Mohochi anasema kuwa hadithi za kwanza kuchapishwa katika Kiswahili ni *Hekaya za Abunuwas na Hadithi nyingine* (1935).

Katika utangulizi wa *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) Mbatia naye anaeleza kuwa hadithi fupi za kisasa ni masimulizi yaliyoandikwa kinathari juu ya tajriba fulani ya maisha. Anasema kuwa:

Uti wa mgongo wa hadithi fupi ni hadithi. (uk. 3).

Anamnukuu Forster (1927:42) akisema kuwa:

Hadithi fupi ni masimulizi juu ya matukio yaliyopangwa kama yalivyotukia kiwakati.

Hivyo basi masimulizi ni msingi wa utanzu wa hadithi fupi. Pia kufaulu kwa kutunga hadithi fupi kunategemea jinsi msanii anavyoyapanga matukio yake kiwakati.

Wamitila (2002) naye anatoa mwanga zaidi na kuangalia Allan Poe kama mwanzilishi wa hadithi fupi. Allan Poe ni mtunzi hasa wa Kimarekani. Kimsingi Poe amechukuliwa kama mwasisi wa utanzu huu. Mhakiki aliyefahamika kama Brander Mathews ameaminika kuwa ndiye alitumia neno la Kiingereza la "short story" kwa mara ya kwanza.

Utanzu huu umekua na kuchapishwa magazetini. Umekuwa ukichapishwa katika fasihi za lugha nyingine zaidi ikilinganishwa na Kiswahili (Wamitila, 2002:66). Ukuaji wa maendeleo ya utanzu huu unafafanuliwa katika fasihi ya mataifa mengi. Waandishi walianza kuandika hadithi zao na baadaye hadithi hizi zikachapishwa magazetini ili kusomwa na wengi.

Wamitila (2002:67) anasema kuwa:

Hadithi nyingine zilishiriki katika mashindano ya uandishi wa hadithi fupi zilizosomwa katika idhaa za BBC na hatimaye kuchapishwa katika mifululizo ya *Mapenzi Ni kikohozi*, *Kinywa Jumba la Maneno* na *Pavumapo palilie*. Diwani hizi za hadithi fupi ziliweka msingi wa kuandikwa na kuchapishwa kwa hadithi fupi. (uk. 67).

Wamitila anatoa orodha ya diwani zingine zilizochapishwa katika miaka ya sabini kama *Parapanda na hadithi Nyingine* (1974). *Uwike usiwike kutakucha* (1978).

Hadithi fupi zilizochapishwa katika miaka ya themanini ni kama: *Si wazimu si shetani* (1978), Cha S. A. Mohamed, *Dhuluma na hadithi nyingine* cha Barshad na *Tamaa mbele mauti nyuma* cha Banzi. Diwani za hivi karibuni ni kama *Pendo la Heba* (1997) kilichohaririwa na Wafula na Kinge'i, *Mwenda wazimu na hadithi nyingine* (2000) kilichohaririwa na Mbatia, na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) kilichohaririwa na Wamitila. Wamitila anasisitiza kuwa masimulizi ndio msingi wa hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili. Masimulizi haya yalikua na kubadilika kimuundo wa kimtindo na kuwa hadithi fupi.

Katika fasihi ya Kiswahili, ngano za mwanzo, hazikuhusiana kamwe na utamaduni wa kigeni. Hadithi za mwanzo kabisa zilikuja na wageni na baadaye kutafsiriwa katika Kiswahili.

Katika eneo la pwani utamaduni wa wageni unajitokeza. Uislamu unajitokeza katika hadithi zilizotafsiriwa na baadaye kutungwa na Waafrika. Baadhi ya hadithi hizi ni kama vile *Hekaya za Abunuwasi* (1935) zilizosimuliwa na Waswahili kama *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1989). Hadithi zingine za hapo awali, zilitafsiriwa kutoka kwa lugha za kigeni hadi kwa Kiswahili. Hadithi hizi za asili ya kigeni zilikuwa *Alfu lela Ulela* (1928) na *Kisiwa Chenye Hazina* (1929).

Hadithi za hapo kale zilitukuza Uarabu, Uzungu na kuponda Uafrika. Zilikejeli Mwafrika kwa kumwita mjinga. Hadithi hizi baadaye zilishindwa kufanya kazi zilizofanywa na ngano za hapo zamani. Baadaye ilimbidi Mwafrika atunge hadithi ambazo zitamsawiri Mwafrika utamaduni wake na ujumla wa maisha yake katika jamii.

Ilimbidi atunge hadithi ambazo zingetoa hali halisi ya Mwafrika, itikadi zake, mila zake na desturi zake, mazingira yake, hali ya kisiasa, hali ya kiuchumi na yote yaliyomzingira Mwafrika, ili kurejesha na kuiumba upya hali ya Mwafrika iliyodharauliwa na wageni.

Magazeti na majarida yamechangia pakubwa katika maendeleo ya hadithi fupi. Magazeti kama *Mamboleo* na *Taiifa* yalichangia pakubwa kuendeleza hadithi fupi. Baada ya mwaka wa 1970, magazeti ya kibinafsi yaliendeleza kuchapishwa kwa hadithi fupi. Mfano wa hadithi za awali zilichapishwa ni

Parapanda na Hadithi Nyingine (1974). Kuchapisha huku kulifanya hadithi fupi kusomwa na watu wengi.

Wamitila (2002:67) akimnukuu Poe kama mwanzilishi wa utanzu huu anasema:

Hadithi fupi si sura katika riwaya. tukio wala ambacho kinachopolewa katika hadithi fupi au kisa kirefu bali humvutia na kumteka msomai na kumfanva aamini kuwa ingeweza kuharibika ikiwa itakuzwa na kuwa ndefu au kama itafanywa sehemu ya kazi kubwa.

Kutokana na dondoo hili, inadhibitisha kuwa utanzu huu ni wa kipekee na tofauti na tanzu zingine za fasihi na wenye wasifu wa kujitosheleza. Hadithi fupi ikirefushwa basi huwa si hadithi fupi tena. Kinyume na haya hupoteza upekee wake na sura yake kama hadithi fupi. Hivyo basi, hadithi fupi siyo riwaya iliyofupishwa.

Poe aliuchukulia utanzu huu wa hadithi fupi kama chanzo cha gazeti la Amerika. Magazeti haya yaliwapa waandishi fursa ya kuonyesha vipawa vyao katika uandishi wa hadithi fupi. Kila kizazi cha waandishi wa hadithi fupi huwa hasa na mtindo wake. Kwa upande wa hadithi fupi, mtindo huu uliendelea tangu utanzu huu ulipojulikana hadi sasa. Waandishi wa sasa wa hadithi fupi wana uwanja mkubwa wa kuzua na kuiga mawazo na mitindo yao ya hadithi fupi.

Tangu hapo awali, hadithi fupi ziliendelea na baadaye kuchapishwa kwenye vitabu ili kuifikia hadhira kubwa zaidi. Machapisho haya yana hadithi tofauti zilizoandikwa na waandishi tofauti wa Kiswahili. Katika hadithi hizi watunzi wanasawiri maisha ya Mwafrika, hali yake ya sasa hivi, maisha yake, hali ya kisiasa, kiuchumi na hata teknolojia ya sasa.

Historia ya hadithi fupi si ndefu kwa hivyo uhakiki wake si mpana sana katika Kiswahili. Kutokana na sababu hii ni bora kuangalia jinsi wahakiki wengine katika maeneo mengine wameishughulikia ili kuirutubisha historia ya hadithi fupi.

Mphaphlele (1966) anaeleza kuwa tabia ya kutamba hadithi ni tabia ya zamani sana iliyo tumiwa kufunza maadili, kama ilivyo lugha ya binadamu. Binadamu mara kwa mara wamekuwa wakiburudika kutokana kwa kuhadithiana kila wakati maishani. Wamekuwa wakifundishana kwa kuhadithiana, huku wamekaa karibu na moto usiku katika sherehe mbali mbali na hata wakiwa katika harakati zao za kila siku.

Tangu hapo zamani, kuna watu ambao wanajua kutamba hadithi. Sifa hii hutokana na ujuzi huu wa kutambiana, kila mara huipa hadithi ule uzuri na urembo wake. Hata hivyo Mphaphlele anaeleza kuwa hali ya kutambiana hadithi kwa njia ya mdomo, inayojulikana kama "fasihi simulizi" inaendelea kufa. Anafafanua kuwa kifo hiki kinatokana na maendeleo ya sasa. Shughuli za wakati wetu haziwezi kutupa fursa ya kuketi na kutambiana hadithi.

Hapo zamani watu waliishi pamoja wakishirikiana kama jamii moja. Sasa hivi uhusiano huu haupo tena kwa sababu ya shughuli na mabadiliko ya jamii. Kando na haya, Mphahlele anasisitiza kuwa kuhadithiana bado kupo. Tunapokutana na watu tusiowajua, kila mara tutajikuta tukihadithiana kuhusu jambo hili au lile. Hadithi inaendelezwa kutokana na kuzuka kwa mbinu nyingine za kuhadithiana. Hivyo ndivyo hadithi fupi iliyoandikwa ilivyoanza.

Naye Grandsaigne (1985) anaeleza kuwa hadithi fupi ilitungwa wakati wa jioni siku moja na mtambaji. Anatambua kuwa binadamu hupenda kutambiana hadithi. Kwa sababu hii hadithi fupi ilizuka. Hata sasa katika jamii ambayo fasihi simulizi inaendelea kuwepo hadithi bado hutambwa na watu.

Grandsaigne(1985:1)anasema kuwa:

katika uropa, hadithi katika maandishi ilianza katika karne ya kumi na mbili, na wale waandishi wa Riwaya. Hadithi ndefu humhusu shujaa mmoja anyetafuta ukweli fulani. Hadithi hizi zilikuwa katika watu wa kiwango cha juu. (uk.1)

Hata hivyo haimaanishi hadithi fupi zilizofupishwa bali ni utanzu unaojisimamia kama tanzu zingine za fasihi. Fauka ya hayo, hadithi zinazoandikwa hata sasa, mara kwa mara, huwa na uhusiano mkubwa sana na fasihi simulizi, ambapo huazima sifa kadhaa kutokana na fasihi simulizi.

(Grandsaigne 1985:1).

Katika Miaka ya Kati, na hata karne zilizofuatwa, tofauti zilijitokeza kati ya masimulizi haya. Katika karne ya kumi na tisa, ndipo hadithi fupi ilijitenga na kuwa utanzu wa kipekee (Grandsaigne 1985)

Mwanzi (1987) naye anasema kuwa hadithi fupi ya Kiafrika ina mizizi yake katika ngano za awali. Anasema kuwa;

Ngano husimuliwa kwa dakika ishirini kumi au hata dakika chache. Ngano hizi ndio msingi hasa wa hadithi fupi(uk.1).

Mwanzi anaendelea kusema kuwa hadithi fupi nzuri ni ile ambayo msimulizi au mwandishi ana hamu ya kusimulia kwa ufupi na kwa njia inayovutia sana. Mwanzi anaelekeza kuwa mzizi wa hadithi fupi ni masimulizi ya hapo awali ambayo yamekuwa na kuendelea hadi sasa.

Katika fasihi ya Kimagharibi, Grandsaigne (1985) anamtambua Poe kama mwandishi wa hadithi fupi aliyefafanua hasa maana ya hadithi fupi na kuweka msingi wa hadithi fupi. Poe anajulikana kama baba wa hadithi fupi ya kisasa.

Kutokana na maendeleo ya jamii, kila uchao hadithi fupi pia ziliendelezwa na kuendelea kubadilika. Grandsaigne (1985) anatambua kuwa fanani wa fasihi simulizi wa hapo awali alikumbana na hadhira yake ana kwa ana kuliko kama ilivyo sasa. Hivyo basi, hadithi fupi iliendelea huku ikibadilika. Katika karne ya kumi na tisa, hadithi fupi ilijisimamia na kujitenga kama utanzu wa kipekee, ambao una sifa zake tofauti na tanzu zingine.

Maudhui yanayozungumziwa na waandishi wa sasa siyo kama ya hapo awali, bali kwa vile mabadiliko yametokea, tangu hapo mwanzo, hivyo basi hadithi hizi zimebadilika. Zimelenga hali ya sasa hivi, maendeleo ya jamii katika siasa, teknolojia, hali ya kiuchumi na jinsi yanavyoathiri binadamu wa sasa hivi.

Wahusika wa hapo mwanzo waliotumiwa katika hadithi wanatumia hata sasa. Siyo kwamba tuyasahau yale ya zamani bali ya zamani yaangaze ya sasa na yajayo. Waandishi hawa hawakupuuza yale ya zamani, bali waliyatumia na kuyaweka katika muktadha wa hali halisi ya maisha sasa hivi, ili kuyasawiri maisha ya sasa hivi ya binadamu. Hadithi fupi za kisasa zimeumbwa kutokana na ujumi na urembo wa umbuji na uchache wa maneno ambayo mtunzi hutumia ili kuelezea wazo au tukio moja katika hadithi yake. Kutokana na maelezo haya hasa katika muktadha wa Kiafrika hadithi fupi imeendelea kistari kutokana na fasihi. Maoni yetu ni kwamba huu si ukweli wa mambo. Ukweli wa mambo ni kwa kuna mwingiliano kati ya sifa za uandishi na sifa za usimulizi. Katika sehemu inayofuata tunazitalii hizi sifa.

2.2 USIMULIZI NA UANDISHI

Usimulizi na uandishi ni mbinu ambazo zimetumika katika jamii tangu hapo zamani na hata sasa. Usimulizi ni mbinu ambayo inahusu neno linalosemwa kwa kutumia mdomo, au maongezi ya kawaida. Kwa upande mwingine uandishi ni mbinu inayoshughulikia maandishi, maneno, sauti na mtiririko wa maneno haya katika matini iliyoandikwa.

Kwa mujibu Ong (1982:9),

Uandishi haukudidimiza usimulizi, bali ulirutubisha na kuweza kuwasilisha vipengele vyake kwa njia ya kisayansi.

Kutokana na wazo kuwa tamaduni za usimulizi ni duni kuliko za uandishi hili wazo halina mashiko. Mbinu hizi zote zina umuhimu katika jamii ya sasa hivi. Mbinu hizi huwa kama wasafiri wanaoenda kwa gari moja. Mbele (1982:3) anasema kuwa;

“Uandishi umekuja kujiunga pamoja na usimulizi katika mawasiliano”.(tafsiri ya mtafiti).

Maoni yetu ni kwamba mbinu hizi mbili, uandishi na usimulizi huenda sambamba katika hali ya kawaida. Mbinu hizi zina sifa zake katika hali yoyote ile. Katika sehemu zifuatazo tutachunguza baadhi ya sifa zinazopatikana katika masimulizi na maandishi. Kwa kufanya hivyo, tutashadidia msimamo wetu kuwa masimulizi na maandishi huenda pamoja. Baadhi ya sifa za masimulizi ni kuongezea, uziada, umbo, matumizi ya methali na vitendawili, kukaribia maisha ya binadamu, nyimbo na kutokamilika.

2.2.1. KUONGEZEZA

Katika usimulizi kuna sifa ya kuongezea na siyo tegemezi katika uandishi. Kwa mujibu wa Ong (1982) maelezo ya Biblia kutoka kitabu cha Mwanzo yanasema hivi:

Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na ulimwengu.
Hamkuwa na chochote na giza ilikuwa juu ya

ulimwengu, na roho wa Mungu alitembea juu ya maji. Na Mungu akasema kuwe na mwangaza na kukawa na mwangaza na akasema mwangaza ni mzuri, na akatenganisha mwangaza na giza na giza usiku(uk. 126).

Katika maoni ya Ong, hali ya kuongeza kwa kutumia “na” inadhihirika zaidi katika usimulizi. Ong anaendelea kusema kwamba katika uandishi hali ya kuongezea kwa kutumia “na” hupunguzwa. Mawazo hufufulizwa na mawazo hujitegemea. Ong anatoa mfano kutoka kwa tafsiri za Biblia zilizofuatia ili kudhibitisha madai haya:

Hapo mwanzo, Mungu alipoumba ulimwengu. Ulimwengu ulikuwa bila chochote. Roho wa Mungu alitembea juu ya maji Mungu akasema kuwe na mwangaza, na kukawa na mwangaza. Mungu akatenganisha mwangaza na giza. Mungu akaita Mwangaza mchana na giza usiku. Hivyo basi kulikuwa na jioni na asubuhi.

Kutokana na maoni haya uandishi huendelezwa kwa njia isiyobadilika na kwa mapana ili kuwasilisha maana. Uandishi hutegemea vipengele vya kiisimu ili kukamilika.

Kwa maoni yetu mikakati ya usimulizi haijabakia vile vile. Imekuwa ikibadilika katika mpito wa wakati. Kwa hivyo maoni yetu ni kwamba, maoni ya Ong huenda yakaonyesha viwango mbalimbali vya usimulizi na uandishi katika jamii ya binadamu.

2.2.2 UZIADA AU YASIOHITAJIKA

Kwa mujibu wa Ong (1982:39), sifa nyingine ya usimulizi ni uziada au "yasiyohitajika". Hali hii ya uziada na kuongezea yale yasiyohitajika, ni hali ya kawaida ya maongezi na hata akili. Kwa sababu ya uziada huu, uradidi hujitokeza mara kwa mara. Uradidi huu hujitokeza wa ili kuhakikisha kuwa msikilizaji au msomaji na msemaji wanawasiliana. Sifa ya uradidi, inazingatia kurudiarudia yale yasiyohitajika. Uradidi huu pia hujitokeza katika uandishi. Finnegan (1970) anasisitiza kuwa uradidi huu hutokea ili mtambaji aweze kuisitiza jambo fulani. Uradidi ulitumiwa katika usimulizi wa ngano za hapo awali, ili kuhuisha yale yaliyozungumziwa. Nyanya angewaambia wajukuu wake hivi "mzee kobe alienda, akaenda, akaenda hadi akafika kwenye lango". Uradidi wa kuenda umerudiwa ili kujenga taswira akilini mwa msomaji au msikilizaji kuhusu kitendo kile. Kwa upande mwingine Ong anasema kwamba, katika uandishi mawazo yasiyohitajika huwa hayatumiwi. Mawazo yanayotolewa huwa ya kistari tu, bila kuhusisha ule uradidi wa yale yasiyohitajika. Lakini kando na mawazo ya Ong, wakati mwingine uradidi pia hutumiwa kwa mfano katika ushairi. Kule kurudia kibwagizo ni uradidi. Msomaji hurudiarudia kibwagizo ili aelewe maudhui. Tumelitalii jambo hili katika hadithi fupi katika sura ya tatu.

Katika uandishi, Ong anasema hali hii ya mawazo yasiyohitajika huwa hayatumiwi. Mawazo yanayotolewa huwa ya kistari tu bila kuhusisha ule uradidi wa yale yasiyohitajika. Iwapo kobe alitembea kwa muda mrefu, basi sifa ya kurudirudia haitakuwepo tena. Hivyo basi, taswira hiyo haitajengeka kama

ya usimulizi bali itajengeka mawazoni mwa msikilizaji au msomaji. Katika baadhi ya hadithi tulizohakiki hali hii ya uradidi imo kuonyesha mwingiliano kati ya sifa za fasihi simulizi na fasihi andishi.

2.2.3 UMBO

Kwa mujibu wa wamitila (2003), Sifa nyingine ya usimulizi ambayo ni ya wazi ni umbo. Umbo la ngano za hapo awali hujitokeza. Fomula ya “paukwa pakawa” “wakaishi raha mstarehe” ina mizizi yake katika masimulizi ya hapo kale. Hata hivyo umbo hili limetumiwa na waandishi. Shaaban Robert katika *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1968) anatumia fomula ambazo zimepatikana katika usimulizi. Usimulizi huu hurejelea kwa mtiririko wa utangulizi, yaliyotokea, suluhisho, na baadaye hitimisho.

Ploti ya masimulizi huendelezwa hatua kwa hatua hadi mwisho. Katika uandishi sifa hii haijitokezi. Mwandishi anaweza kuanza na mwisho ndipo baadaye arejeele mwanzo. Ngure (2003) anauita mtindo wa fasihi simulizi wa “kikasuku” yaani mtindo wa kuiga tu. Mtindo huu unatofautiana na ule wa usimulizi ambao una mtiririko unaodhihirika.

Kwa mujibu wa Lord B. A. (2000) katika matini ambayo ni ya usimulizi, kuna maelezo fulani ambayo yanajitokeza kwa utaratibu. Lord anadai kwamba Katika uandishi hakuna utaratibu huu au iwapo upo, utaratibu huo basi ni machache sana. Hata hivyo mbinu hii hutokea katika uandishi.

2.2.4 MATUMIZI YA METHALI NA VITENDAWILI

Usimulizi una sifa ya matumizi ya methali na vitendawili. Methali, utani, vitendawili na hata vichekesho huwa na asili yake katika fasihi simulizi hasa ngano za hapo awali. Harson anasema (1978:25):

Kama vile chumvi huipa ladha chakula, vivyo hivyo methali huyapa ladha mazungumzo

Ong (1982) anasisitiza kwamba methali na vitendawili huwapa hadhira fursa ya kushiriki katika masimulizi kimaongezi na hata kimaarifa. Kutamka kwa methali au kitendawili humpa msikilizaji au msomaji changamoto ya kujaza na lingine ambalo ni kinyume ya yale yaliyosemwa.

Ong anaongezea kusema kwamba mivutano ya nje hushughulikiwa na usimulizi na wala si uandishi. Kufuata mila na desturi ni sifa nyingine inayojitokeza na kusisitizwa. Katika usimulizi, mila na desturi huwa na misingi yao. Siyo kwamba katika masimulizi, hadithi mpya huumbwa bali, ni hali ya kuleta uhusiano kati ya hadhira yake mtambaji na wakati huo. Kila hadithi huwa inaanzishwa kwa njia tofauti kulingana na mazingira. Msimulizi huongeza mapya kwenye hadithi ambayo ni ya hapo kale ili kuafiki wakati huo.

Kwa mujibu wa Ong 1982:44 anasema;

Katika jamii za usimulizi visasili, visakale hubadilishwa kwa kiasi kidogo. Hata hivyo marudio yatakuwepo. Uradidi utakuwepo. (tafsiri ya mtafiti).

Maudhui ya hapo kale, yanahusishwa na hali ya sasa kijamii, kisiasa, kiuchumi na hivyo mitindo ya hapo awali hutumiwa na kubadilishwa kuafiki mazingira ya sasa.

Akirejelea maudhui ya "mama wakambo" Ong anasema yalikuwepo tangu jadi. Sasa hivi maudhui haya hubadilishwa kuafiki hali ya uyatima ambayo hata sasa hali hii ya uyatima ipo, ikawa na mizizi yake katika ngano za hapo kale. Katika uandishi hali ya kutiliwa mkazo mila, desturi na tamaduni pia ipo. Uandishi unatumia utamaduni na mizizi yake Hivi ni kusema kwamba mbinu hizi huenda sambamba. Matumizi ya methali na vitendawili hugemea muktadha uwe wa usimulizi au wa uandishi.

2.2.5 KUKARIBIA MAISHA YA BINADAMU

Sifa nyingine iliyo wazi katika usimuliaji ni kule kukaribia maisha ya binadamu. Maisha ya binadamu ya kila siku yanahusu hali nyingi anazopigana nazo mtu kila kuchao. Tamaduni za usimulizi hutamka ujuzi wao huku wakizingatia tabia, vyombo, na maisha ya kila siku ya wanyama na yale ya binadamu. Iwapo ni wanyama wanaotumiwa watapewa majina ambayo yanawatambulisha katika hali halisi ya binadamu na ambao wamo katika mazingira halisi ya binadamu. Tamaduni za uandishi mara nyingi hurejelea vitu ambavyo havipo katika maisha halisi ya binadamu. Ong (1982:43) anasema utapata mambo haya katika usimulizi;

Katika tamaduni hizi, hakuna jambo la jinsi ya kufanya kitu, miongozo ya kufanya jambo fulani.

Miongozo ya kufanya jambo fulani haipatikani katika tamaduni hizi za usimulizi, bali mambo hutendeka kikawaida. Jinsi maisha ya binadamu yanavyoendeshwa ndivyo mambo yalivyo. Kwa upande mwingine, uandishi huweza kusimulia visa ambavyo vipo mbali na binadamu, hasa jamii ya wakati huo. Kwa mfano, gari laweza kujiendesha, likifika mwisho, likajiegsha kungoja kuendelea na safari. Hali hii siyo ya kawaida ya binadamu jinsi wanavyoifahamu. Hata hivyo mambo haya hayapatikani katika uandishi pekee bali pia katika usimulizi. Ong (1982:43) anatoa mfano akisema:

Sasa hivi meli nyeusi, songa pale kwenye ziwa
kubwa lenye chumvi.

Ni vipi ambavyo meli itaelezwa kusonga na hivyo basi ikasonga. Hali hiyo siyo inayomkaribia binadamu na maisha yake halisi. Kwa hakika hali hii ni jambo linalopatikana zaidi katika mapokeo ya usimulizi.

Sifa hii ya kidhahania na kujitenga na vitu, vifaa, wanyama katika mazingira halisi ya binadamu, inahusu hisia, hali ambayo si ya kawaida na huzua ulimwengu ambao haupo, bali unaotarajiwa kuwepo. Tamaduni za usimulizi hazitazami ujuzi na maarifa ya vitu vilivyo vya kidhahania, vilivyojitenga na ulimwengu. Zinahusisha mambo haya yote na mambo halisi yanayotendeka katika maisha. Iwapo kiongozi mmoja aliishi, akawaongoza watu, akaenda vitani, akapigana na kikundi cha watu wakati fulani akatumia mikuki, hilo ndilo litakalosemwa katika usimulizi huu ili kuhusisha hali hiyo na hali halisi ya binadamu. Mazungumzo ni hali ya kawaida ya usimulizi. Wahusika

huwasiliana kwa sauti na maneno. Viumbe ambavyo si asili ya binadamu hupewa uwezo wa kuzungumza.

Mazungumzo huibua picha halisi sana kuliko maendelezo ya mawazo moja kwa moja, jinsi inavyojitokeza katika uandishi. Kwa mujibu wa Miruka (1994:178):

Mazungumzo huwafanya wahusika kuwa katika hali ya kweli na wanayohusiana.

Mazungumzo husema zaidi juu ya tabia ya wahusika katika usimulizi wowote. Schwiebert (2001) anaeleza kuwa mazungumzo hueleza uhusika wa wahusika kwa njia ya wazi na hutumiwa kuendeleza ploti ya hadithi. Mazungumzo ni majibizano ya moja kwa moja. Huibua hisia za machungu na furaha ya wahusika huku wakijibizana.

Katika utamaduni wa uandishi maelezo ya moja kwa moja sentensi zilizokamilika na kutoa hoja moja kwa moja. Mazungumzo huvunja ule mtiririko wa uandishi. Hata hivyo usimulizi na uandishi hujaribu kukaribia maisha ya binadamu lakini mazungumzo pia hupatikana katika uandishi.

2.2.6 NYIMBO

Nyimbo humleta msomaji karibu sana na yale masimulizi aliyotaka kuyasema. Usimulizi utahusu nyimbo ambazo zitawapa uhai wahusika na kuzua mawazo yao. Nyimbo pia huweza kuonyesha uhusiano wa wahusika hata pale pasipo mazungumzo. Miruka (1994) anasisitiza kuwa nyimbo huzalisha maudhui ya kazi ya fasihi. Nyimbo zinapotumiwa, maudhui na ujumbe hubainika zaidi

katika maneno ya nyimbo hizo. Nyimbo hutumiwa kama sifa moja ya usimulizi ili kupunguza uchovu wa maelezo ya moja kwa moja kama ilivyo katika uandishi. Gibbe na Mvungi (1987:9) wanasema kuwa:

Baadhi ya nyimbo za fasihi simulizi zinahusu makatazo. Yaani, zinawakataza wanajamii kutenda mambo fulani ambayo si mazuri katika jamii"

Hivyo basi, nyimbo hutumiwa kama onyo ili kusisitiza maudhui ya usimulizi. Nyimbo hutumiwa vilevile katika uandishi. Kabla ya kuimbwa, nyimbo huandikwa ndipo zikaimbwa. Swala hili linadhibitisha kwamba usimulizi na uandishi huenda sambamba.

2.2.6 KUTOKAMILIKA

Sifa nyingine ni kutokamilika kwa sentensi na maelezo yasiyo na mpangilio. Kwa mujibu wa Mbele (1982), sifa hii huwa haivurugi uchanganuzi wowote wa matini kwa sababu sifa hii inafidiwa na sifa zingine ambazo si za kiisimu.

Katika kutokamilika au kutopangika vilivyo, hadithi huenda isikamilike. Hadithi inaposimuliwa, fanani huenda akatamba, anapofika kati kati, akaongeza kitu kingine tofauti na hadithi hiyo, na baadaye akairejelea. Hali hii hujitokeza katika masimulizi. Hata hivyo haivunji kuelewa kwa hadithi hiyo. Anapoendelea kusimulia, huenda akasema neno na asimalizie au pia ayaondoe maneno mengine. Hali hii ni sifa inayojitokeza katika usimulizi ili kuwafanya wanaosikiliza kuwa makini sana.

Anaweza kusema:

safari hiyo iliendelea kwa muda mrefu sana na tulipofika hapo tuliwaona simba waliokuwa tayari kutuvamia. wakati huo...

Ataiachia hapo ili anayesikiliza aweze kujijazia na kutabiri yatakayotendeka baadaye. Kwa kawaida, uandishi utaendeleza mawazo yake kwa mpangilio ulio na mtiririko. Mwandishi huratibu mawazo yake moja kwa moja, bila kuyaweka kiholelaholela ili yaweze kuzua maana iliyokusudiwa. Mtiririko huo utakamilika kwa kutumia vipengele vya kiisimu na sheria za kiisimu ili kukamilisha mawazo yake. Hata hivyo hali ya taharuki hupatikana katika uandishi na usimulizi.

2.3 HITIMISHO

Ingawa baadhi ya wataalamu wanasema sifa za usimulizi ni za kipekee, sifa hizi zinaingiliana na sifa za uandishi. Finnegan (1970:19) anasema kuwa:

Vipengele vya fasihi simulizi vimetumiwa katika fasihi andishi, na hata fasihi simulizi ipo tayari kutumia vipengele vya fasihi andishi yakiwemo maandishi. (tafsiri ya mtafiti)

Vipengele vingi vya usimulizi huenda vimetoweka lakini kila wakati vingine vya kimahuluti huibuka na hutumiwa pamoja na uandishi. Mbele (1982:2) asema hivi:

Fasihi simulizi na andishi zimekuwa tamaduni ambazo ni kama abiria wanaosafiri katika gari moja.

Usimulizi na uandishi katika ulimwengu wa sasa huambatana na kuzua kazi iliyo mahuluti. Umahuluti huu hutokana na kule kuchangiana kwa mbinu hizi mbili za fasihi. Jambo hili limempelekea mtafiti kuzungumzia umaluhuti na jinsi unavyojitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Katika sura ifuatayo tutachanganua umahuluti wa hadithi fipi za kisasa za Kiswahili kwa mujibu wa maelezo tuliyotoa hapo juu.

SURA YA TATU

3.0 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita tuliangazia sifa za usimulizi na uandishi kwa ujumla. Usimulizi ni mbinu ambayo inahusu neno lilosemwa kwa kutumia mdomo. Katika sura hii tutaainisha na kuchanganua sifa hizi za usimulizi huku tukizingatia machapisho tuliyoyachagua hapo awali.

Tutaangalia sifa hizi za usimulizi katika machapisho ya *Pendo La Heba* (1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Sifa hizi ni mazungumzo, matumizi ya methali, matumizi ya monolojia, matumizi ya nyimbo miongoni mwa sifa zingine za usimulizi. Sifa hizi zinapatikana katika usimulizi na hata uandishi.

3.1 MAZUNGUMZO

Fasihi simulizi mara nyingi hutufanya kufurahia urembo wa lugha kwa uneni. Ngure (2003) anasema fasihi simulizi hutufanya kufurahia na kuiheshimu lugha hasa uneni. Uneni huu huweka wazi wahusika na uhusika. Kando na haya, mazungumzo kuweka wazi zaidi maudhui ya mwandishi kando na maelezo ya moja kwa moja. Haya mazungumzo hutumiwa sambamba na maelezo ya moja kwa moja.

Mazungumzo yametumiwa katika hadithi ya “pendo la heba”, hadithi ambayo inahusu ndoa na matatizo ya ndoa katika jamii ya sasa. Hadithi hii inapatikana katika kusanyiko la hadithi fupi la *Pendo La_Heba na Hadithi Nyingine* (2000). Mazungumzo kati ya Pesa na Musa katika hadithi hii yanaonyesha mawazo mazito aliyonayo Musa kuhusu ndoa yake.

“Baba Mbotela, kuna simu, labda mama Mbotela ndiye apigae.
 Aliahidi kupiga”
 Okay”, akajibu
 Moyo ukiwa unamdunda na masikio katega, aliuliza
 “hallo?”
 Hallo” akajibiwa
 “Napiga kukuuliza kama hapo ni kwa Lea Mkapi, nina
 ujumbe wake kutoka kwa Jane,”
 Akaendelea.
 “Hayuko Lea Musa”
 Alimwambia
 “Ninaweza kuwacha ujumbe”
 “Ukipenda”
 “Haya mwambie tukutane Jumamosi katika mtaa wa Jambo
 ili tutayarishe mipango yetu ya wanawake . Mwambie hivyo
 ndivyo Jane alivyotaka nimwambie. (uk.2).

Mazungumzo haya yanasisitiza wasiwasi ambao ulikuwa rohoni mwa Musa kuhusu ndoa yao. Anapozungumza roho ikimdunda ni kwa sababu ya hali ya kutokuwa na uhakika na ndoa yao. Mazungumzo mengine yanajitokeza baina ya Musa na daktari aliyemtembelea.

Bwana Musa Mukapi alimuuliza
 “La sivyo lakini---”
 “Lakini nini”

Daktari Musa ambaye alikuwa fundi wa maneno alidakia usemi

“Ah” wewe Bw. Musa nimckuja kukushauri kimoja

“Nini?” Bw Musa akamwuliza.

“Mambo ya mke wangu yamenishinda. Kila siku ananitilia uchoro na hata nikifanya nini simuridhishi. Hili ni juma la nne hatujazungumza wala kuambiana la heri au la shari. Kila mmoja wetu yuwajishikia hamsini zake. Najipikia mwenyewe na yeye hata hashughuliki.”

(uk.4).

Mazungumzo haya yanazua hisia na mawazo aliyonayo daktari kuhusu ndoa yake. Ndoa yake imeendelea kuwa mbaya hadi kiasi cha kujipikia na mkewe hajali. Mazungumzo pia yanayozua maudhui ya kutojali baina ya Lea na Bwana waziri (uk. 5-6).

“Waonaje huku, binti?” Bw. Waziri aliuliza

“Aaa fit sana” alisema Lea

Ni kweli naona mazingira, watu mimea, mito, hali ya hewa”, Waziri- aliendelea

“Mimi ningependa niishi huku, maisha yangu yote.

“Lakini tumetumwa na serikali yetu kumbuka” waziri alitahadharisha Lea akiwa ameshikwa na haya akasema

“Hilo ndilo, labda litakalonifanya kurudi”

“Huku ukibaki utaishi na nani?,” Waziri aliuliza

Watu”, akajibu Lea akichekacheka kama msichana wa miaka kumi na minane”.

“Mume wako atakasirika”

Sina deni lake mimi, tunaishi tu. This is my chance to be away from him.”

(uk. 5-6)

Mazungumzo haya, yanaibua hisia za Lea kuhusu ndoa yake. Yeye anaona hana deni aliloacha kule Kenya na hana deni na Musa. Huku ni kukosa uaminifu katika ndoa za kisasa. Lea hajali maisha ya ndoa yake, bali yeye hana haja na Mume aliyemwacha na watoto.

Kwa mjibu wa maelezo haya Muriithi (2002) anasema kuwa mazungumzo huelezca hisia na matamano ya wahusika, na kumwezesha msimulizi kumwelewa mhusika zaidi. Anaendelea kueleza kuwa mazungumzo huweza kuwa ya ana kwa ana au ya simu. Mazungumzo ya ana kwa ana mara nyingi hayana mpangilio, na utaratibu wowote. Kuna uwezekano wa kuchanganya ndimi.

Lea anapoongea na mkubwa wake katika hadithi ya “Pendo la Heba” anachanganya ndimi, anasema:

“Sina deni lake mimi. Tunaishi tu. This is my chance to be away from him”.

“Vipi? Una maana gani, binti?”

Aliuliza Waziri

“Huyo nilimsahau siku nulikuwa nikitoka Kenya na sijamfikiria”
(uk.7)

Huku kuchanganya ndimi mara nyingi, huashiria watu waliosoma au wenye vyeo vya juu katika jamii. Katika mazungumzo, mada huweza ikabadilishwa, sentensi huweza ikakatwa hivyo basi hazikamiliki. Sifa hii ni sifa ya usimulizi na hata hivyo inapatikana katika uandishi vilevile. Mazungumzo huibua maudhui ya mwandishi na kuyaweka wazi. Mazungumzo huelezca zaidi mawazo na hisia za wahusika. Mazungumzo yanatokea kati ya Agnes na Onesmas katika hadithi ya “pendo la heba,” katika chapisho la hadithi fupi la *Pendo La Heba* (1997). Agnes Anapofika Nairobi, anakaribishwa vizuri na mumewe na anamuuliza amwambie ni siku ipi atakayorejea nyumbani.

Nirudi nikafanye nini? Kanu alikuja juu

Ukalce watoto

Sirudi

kwa nini?

Fanya mpango uwalete huku. Itakuwaje watoto walelewe na mzazi mmoja, hali wazazi wote wako hai?

(uk. 30)

Ngoloso hakuendelea na mjadala huo. Mazungumzo haya yalikuwa wazi, maudhui ya kutoaminiana kati ya Ngoloso na Agnes. Ngoloso alihitaji muda wa kuweza kuishi maisha yake huku wakihusiana na Faith. Sentensi fupi fupi zimetumiwa katika mazungumzo haya kuonyesha kule kujibizana kati ya Ngoloso na Agnes. Agnes pia anaendelea kutumia maswali ya balagha ili kuzua taharuki iliyomo akilini mwake. Maswali haya yanamwezesha msomaji kutafakari zaidi kuhusu hali ya ndoa baina ya Ngoloso na Agnes. Maswali haya yanaulizwa kwa minajili ya kuelewa zaidi hali na uchungu alionao Agnes. Anaulizwa hivi.

Ni mwanamke gani huyu ninayesikia mnaishi naye?

Mbona usimuo kabisa umlete nyumbani aonekane na kila mtu?

Unaficha nini? Au ni malaya umeokota huku?

(uk. 30)

Anarudiarudia maswali yake kwa njia tofauti. Kurudia huku ni kwa ajili ya kusisitiza na kuweka wazi hali yake. Hali hii inasisitiza hali ya mazungumzo katika uandishi vile vile inavyotumiwa katika usimulizi kusisitiza maudhui. Mazungumzo mengine ni baina ya Faith na Ngoloso aliye mkubwa wake. Katika hadithi ya "Korti ya kishenzi" katika *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000)

Unaumwa na nini? Ngoloso alimuuliza
 Sina neno
 Ngoloso alifululiza hadi afisini, akitikisa kichwa
 chake. Alihisi kuwa kuna kitu cha kumsumbua mpenzi
 wake. Alipiga simu akamuomba akapite ndani.
 Faith una nini Leo Mpenzi? alimuuliza mara tu alipoingia
 na kuketi.
 Sina neno bwana Ngoloso alikariri jawabu lilelile.
 Sauti yake ilikuwa na urasmi ambao haukumpendeza
 bwana boshi wake.
 Nilitaka twende lunch. Labda itakuchangamsha.
 Tutazungumza zaidi huko
 Sijisikii
 Ngoloso hakuyaamini masikio yake.

(uk. 33)

Hali ya Faith ilikuwa ya kuhofia maana alikuwa na mazito na machungu
 yaliyokuwa rohoni mwake. Haya yalikuwa rohoni mwake baada ya
 kuisoma barua hii. Mazungumzo zaidi yanajitokeza baina ya wazee
 waliotumwa kwa Ngoloso, Uk 37-38. Hayana mtiririko wa moja kwa
 moja. Haya pia yanaibua uchungu waliokuwa nao wazee hawa kwa
 sababu ya vitendo vya Ngoloso.

Mazungumzo haya yanaelezea zaidi tabia ya Ngoloso ya kutowatii wazee.
 Ngoloso alikosa utu, kiasi cha kuwaitia Askari. Majibizano mengine ni
 kati ya Ngoloso na wajumbe waliotumwa kwake. Mazungumzo haya
 yanatuonyesha adhabu kali aliyoipata Ngoloso kwa kutowatii wazee.
 Yanaonyesha machungu aliyoyapitia Ngoloso. Hakusamehewa kamwe
 bali alipigwa, vikali ili kutambua makosa yake.

Maswali yametumiwa katika mazungumzo haya. Maswali haya yametumiwa ili kuendeleza hali ya majibizano kati ya Ngoloso na wajumbe wake. Maswali haya yametumiwa kuisisitiza usimulizi na hali yake anaposisitiza maudhui yake. Vivyo hivyo katika uandishi huu yametumiwa kurutubisha maudhui ya mwandishi. Maudhui ya kutotii yanajitokeza na hivyo tunagundua Ngoloso aliacha mila na desturi zake. Hivyo sasa akawa kama mtumwa. Maswali haya hata ingawa ni sehemu ya usimulizi yameingizwa katika uandishi.

Mazungumzo huwasilisha moja kwa moja hisia za wahusika wenyewe. Mazungumzo yanamwezesha msomaji kumwelewa mhusika fulani, kwa vile mhusika huyo hufichuliwa vizuri. Mazungumzo pia huonyesha hali ya kihisia aliyonayo. Huonyesha mvutano alinao mhusika.

Wamitila (2002: 60) anasema:

Lugha ya binadamu huwa na mikatizo mingi na huonyesha ukosekano wa mshikamano. Mara kwa mara tunasita katika maongezi yetu; tukitafuta neno linalofaa na wakati mwingine tunashindwa kusema lolote.

(uk. 60)

Kawaida ya mazungumzo huwa na tabia ya kukatiza usemi. Mazungumzo ni sifa moja ya usimulizi inayopunguza machovu ya kusoma aya ndefu ndefu za kazi ya fasihi. Katika hadithi ya Arusi, katika *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000), Mazungumzo kati ya

Muriti na Kanana yanaibua hisia tofauti sana akilini mwa msomaji.

Mazungumzo haya yanatufunulia dhima ya wahusika hawa.

We ni mgeni sana huku ama? *Alitazua*

Kanana alitabasamu, tabasamu ambalo Muriti alilionna kama kuchanua au kwa uzuri na uvutiaji wake, kisha akajibu kwa kuuliza

Kwa nini wasema hivyo?

Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kukuona leo; na... naweza kusema kuwa nawafahamu watu wazima wote wa vijiji jirani, hasa wasichana wazuri.

Kanana alicheka, moyo wa Muriti ukaanza kupiga kama ngoma kifuani mwake, kana kwamba ukitaka kufunguliwa utoke nje, umwone huyo Kanana mwenye kicheko kuzuri kama hicho.

(uk. 15)

Mazungumzo haya yaliendelea kutufunulia sifa ya hawa wawili.

Walizungumza huku wakichanganya ndimi. Kuchanganya huku

kulionyesha kiwango chao cha elimu.

Mazungumzo mengine yaliibuka kati ya Muriti na babake. Anampa wosia

mtoto wake, asimwoe msichana huyu. Naye Muriti hataki kuyasikia haya

bali anataka kumwoa msichana huyo.

Baadaye babake anamwambia hivi:

Ukimwoa wewe si mwanangu tena, Mzee alifoka

ukinikataza kumuoa, basi wewe si babangu tena,

Muriti alitamka kwa hamaki na kutoka nje.

(uk. 25)

Mazungumzo haya yanaonyesha wazi kutoclewana kati ya Muriti na babaye kuhusu suala la ndoa. Muriti anakataa wosia wa babake, na mwishowe akapatwa na janga kubwa maishani. Mazungumzo mengine yanajitokeza katika ukurasa wa 15,16,18,19 na 26. Mazungumzo haya yanahusu wahusika na matarajio yao maishani. Mengine yanaishilia kukamilika, lakini mengine hayakamiliki.

Mazungumzo ni sifa bayana katika usimulizi lakini pia hujitokeza katika uandishi. Mazungumzo yanaonyesha hali na tabia ya wahusika. Katika mazungumzo, kunatokea majibizano baina ya wahusika. Muriithi (2002). Hisi za ndani za wahusika pamoja na matamano ya wahusika yamawekwa wazi kwa kutumia mazungumzo. Mazungumzo ya ana kwa ana huenda yasiwe na mpangilio wowote. Wahusika huenda wakachanganya ndimi. Sentensi huwa za kukatwakatwa. Wahusika huenda wakasisitiza vipengele fulani wanapozungumza. Katika hadithi hii ya "Kipara Ngoto" inayopatikana katika *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000), ina mazungumzo baina ya Matata na ami wake. Mazungumzo haya yanaonyesha kukerwa kwa ami wake Matata. Matata anasoma kitabu cha "Hardly Chase", kwa sauti ya juu. Ami yake anamwambia

"Shaarab! baba alinguruma

inani wewe unageuza nyumba yangu studio ya matangani
radio.

I am sorry uncle” Matata alimtaka radhi ami yake
 Eehl Usiniboboje umombo hapa ushasikia
 Ndiyo ami, matata alijibu kwa unyonge.”

(uk. 62).

Matata alijibu kwa unyonge huu huku akikiri makosa yake ya kutoiheshimu nyumba ya ami yake. Mazungumzo mengine yanaibuka kati ya matata na binamuye. Wanazungumza jinsi matata alivyofukuzwa shule tatu. (uk. 63). Baba yao alikasirika kwa kusikia vicheko vyao. Mengine ni kati ya Matata na binamuye kuhusu yule aliyeasisi jina la “Kipara Ngoto”. Kupitia kwa mazungumzo haya tunaweza kutambua hisia na misimamo ya wahusika hawa wawili. Kupitia kwa mazungumzo yao, kuhusu kufukuzwa shuleni kwa Matata, yeye anaona maovu yote shuleni yanatendwa na wanafunzi. Matata pia amekasirishwa na jinsi wanafunzi wengine wanamwita “kipara ngoto”. Ana bidii ya kumtafuta mwanafunzi aliyeasisi jina hili na ampe adhabu kali. Mazungumzo yametumiwa baada ya matumizi ya aya ili kupunguza uchovu wa kusoma aya. Kupunguza maelezo ya moja kwa moja.

Sifa ya mazungumzo hutumiwa na waandishi ili kurutubisha sifa ya uandishi na kuvunja uchovu wa kusoma maelezo marefu marefu. Sentensi fupi fupi zimetumiwa kuonyesha hali ya akili ya binadamu anaposimulia jambo. Majibizano hujitokeza katika mazungumzo ili

ukweli huo ukamilike. Mhusika anaweza kuzungumza na mchemu au mizimu katika yale mazungumzo. Mtiririko wa sentensi huenda ukapotoka katika mazungumzo. Sentensi fupi fupi huenda zikatumika kuwasilisha ujumbe fulani katika mawasiliano kati ya watu. Mtiririko huu mara nyingi hutokea katika usimulizi ambapo sentensi hukatizwa. Hamna mtiririko mzuri wa sentensi, katika “fumbo la Mwana” kwenye *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Mawasiliano kati ya Nanda na babake yanadhirisha uhusiano kati ya baba na mtoto. Nanda anamletea babake barua kutoka kwa mwalimu mkuu.

“Habari ya jioni baba” aligutushwa na salamu za mwanawe wa kiume Nanda.

“Si mbaya” alijibu huku angali na mzubao wa zile sinzia sinzia zake. “Vipi habari za masomo huko shuleni kwenu?”

“Nzuri tu,” alisema Nanda

“Hii barua yako kanipa mwalimu mkuu”

(uk. 91)

Mazungumzo haya yanaonyesha fikra za mzee na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya mzee Atanasi na Nanda. Sentensi fupi fupi zimetumiwa, lakini mada inacleweka. Mazungumzo kati ya mwalimu mkuu na mzee Atanasi yanaonyesha wasiwasi alionao mwalimu mkuu kwa Nanda. Katika mazungumzo kuna hali ya kutulia kidogo, kwani mazungumzo yanaendelea kukatika katika mawasiliano. Hali hii ni ya usimulizi. Fanani akisimulia mara huenda akanyamaza ili hadhira ijaze alipowacha na baadaye kuendelea. Au pia afikiri kidogo, na baadaye aendeleo.

Mwalimu mkuu anapozungumza na mzee Atanasi, anasitasita, ananyamaza kwa mda akamgonje mzee Atanasi amjibu.

Mzee Atanasi akazinduka “Mwalimu nimecupata wito ...” Lakini kabla hajaendelea mwalimu akamkatiza.

“Naam naam, wewe ndiwe mzee Atanasi Mukasi. babake Nanda?”

“Ndimi”

“Basi mzee nimekutia jambo moja tu. labda dogo tu lakini hata hivyo muhimu”

mhm”

Ni kumhusu mwanao Nanda.... Mh... sijui unamwonaje siku hizi?”

mhm” ... sikuelewi mwalimu

Nimuone..... nimuoneje tena?”

Huoni mabadiliko yoyote katika tabia na mienendo yake! Labda hata hali yake ya kiafya hivi?

(uk 96)

Mazungumzo na kukatiza sentensi ni hali ya usimulizi, hata hivyo.. yametumika katika uandishi kuyaweka maudhui wazi. Mtiririko huo hujitokeza wazi, kwa hivyo mada yaeleweka. Mazungumzo mengine yanaibuka baina ya Nanda na babake mzee Atanasi. Anapogundua aliyekuwa mapipani ni mwanawe, anazungumza kwa uchungu kwa mshangao huku Nandwa akiwa na hofu.

Sentensi fupi fupi zilizokatizwa zinatumiwa kuonyesha hofu na mshangao kati ya mzee Atanasi na mwanawe Nanda (uk.97).Katika usimulizi mazungumzo hutumika kwa kukatizwa ili kuisisitiza hali ya mazingira na hali halisi ya wahusika.

Mazungumzo yana jukumu la kuendeleza msuko, ukuzaji wa wahusika, ufafanuzi wa mandhari na usimulizi. Mazungumzo ni uwasilishaji wa maongezi ya wahusika kwa maneno yao.

Sentensi hukatizwa mara kwa mara katika mazungumzo na mada hubadilishwa katika haya mazungumzo. Bakhtin (1986:81) anaeleza kuwa watu huzungumzia mambo ambayo tayari yamezingatiwa. Hivyo katika mazungumzo hivyo kuna kujibizana. Katika hali ya kujibizana, kunakuwa na mtiririko wa maswali na majibu. Katika hadithi hii, mazungumzo yanazua hali halisi baina ya wahusika. Yametumiwa kuonyesha matamano na hata maoni ya wahusika katika hadithi ili kumwezesha msomaji kuwaelewa wahusika (Muriithi 2002).

Katika hadithi ya "Ngome ya Nafsi," katika chapisho la *Mayai Waziri Wa Maradhi na hadithi nyingine* (2004), kuna mazungumzo baina ya kina mama waliomuona Naseko akichukuliwa na kubebwa na vijana waliotumwa. Tunaona mambo haya yanayowakera kuhusu Naseko.

Kilio ni cha nini sasa? Binti akisha kukoshwa unyago ya nini kumweka nyumbani. Hana budi aende kwa mumewe ati akikataa, hivi ndivyo afanyavyo. Anataka mahari yarudishwe? Kiingiacho kwa mganga hakitoki
Mh! Ajabu ya shingo kukataa kulala kitandani. Mwingine alidakia
Hebu nicheke hehe hee!
Alimsimanga.

(uk. 101)

Mazungumzo haya ni ya wazi kati ya kina mama hawa. Wanatumia sentensi fupi fupi, maswali na hata tanakali sauti wanapocheka. Sifa hizi zote zinadhahirisha sifa za usimulizi. Matamanio yao yanawekwa wazi huku wakishangaa ni vipi Naseko amekataa kutii na kwenda kwa mumewe.

Mazungumzo mengine ni kati ya baba na dada zake Naseko:

“Baba --- babal Ba—”

Samba alianza kutamka, lakini alishindwa kukamilisha maneno yake kwa kuwa pumzi zilizochanganyika na woga zilimpaa, zikamsakama na kumtia kitata cha ulimi.

“N’ Nini? Mbona mnanijia na magudulia matupu? Maji ya wapi?”
Mzee mengo aliwauliza---

“Haya nimesikia sasa rudini kisimani mkateke maji kabla ya jua kutua --- ama nanyi mtafanywa kama yeye” aliwaeleza.

“Lakini baba” alianza Neema, lakini baba yao alimkatiza usemi kwa kuinua mkono wake juu na kusema kwa hamaki “Kisimani haraka!, hayo mengine niachie mimi”(uk 102).

Mazungumzo haya yanaonyesha hali ya kutumia sentensi zilizokatwa katwa. Kule kukatwa kwa sentensi kumeonyesha hali ya dada zake Naseko. Mazungumzo mengine yanajitokeza kati ya mama na watoto katika ukurasa wa (102-103) kuna matumizi ya sentensi fupi fupi na kukatiza mawasiliano.

Mazungumzo mengine ni kati ya Naseko na mzee Sakaja huku akiongea kwa uchungu (uk 107). Kuna mazungumzo mengine kati ya Naseko na kivuli cha mtu aliyekutana naye kichakani (uk 110). Kupitia kwa mazungumzo haya tunaona uoga alionao Naseko.

Mazungumzo mengine yapo kati ya Naseko na bawabu katika uk. 112 na mawasiliano mengine kati ya Naseko na Bi Tesi katika uk. 113. Katika hadithi ya "Msamaria Mwema," iliyomo katika chapisho la *Mayai Waziri Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), Mazungumzo yametumiwa ili kuonyesha hali ya aliyegongwa na mwenye gari. Mazungumzo humfanya msomaji kupata picha halisi ya wahusika na mazingira yao. Muuguzi anauliza mwenye gari kuhusu yale yaliyotendeka.

Kumetokea nini? Yule mwuugwana akijikohoza kikohozi bandia kisha akasema
 "Nini hivi - alitua kisha akamwinamia kidogo kama ndio anamtambua kwa mara ya kwanza. Aliendelea unavyoona ni kama aligongwa. Basi mimi nikamkuta kule anagaragara chini. Unajua zamani nikienda kanisani... Nakumbuka kisa cha msamaria mwema: kufupisha habari mimi ni msamaria mwema niliyemwokota mzee huyu chini. "

(uk 82)

Muuguzi anasema baadaye;

“Una roho nzuri” Dereva aliitikia pongezi hizo
kwa kichwa tu juu chini, kama mjusi kafiri.

(uk.83)

Mazungumzo haya yanaonyesha hisia za dereva huyu huku akidanganya. Yuaendelea kusema yeye ni msamaria mwema ilhali yeye ndiye aliyemgonga. Likono anatumia sentensi fupi fupi, kuonyesha uchungu aliokuwa nao, hata alipoeleza. Mazungumzo mengine yanayotoa utata kwenye ujumbe aliouwasilisha mwenye gari ni mazungumzo ya Likono. Alisema;

Yu --- le - pal -eee,--
Hakuniokota --- yule
Anadanganya ---- (uk 84)

Hivyo basi kutokana na hali yake, Likono aliongea huku akisitasita kwa sababu ya uchungu aliokuwa akiuhisi. Kusita kwa mhusika huzua hali yake halisi. Mtambaji anapoitamba hadithi, yeye husitasita huku akitamba jinsi mhusika wa hadithi alivyokuwa akisema. Mazungumzo mengine ni kati ya wenye gari na rafiki yake walipokuwa wakizungumza kwenye simu (uk.86)

3.2 MATUMIZI YA METHALI

Methali kama masimulizi ya moja kwa moja zimetumiwa. Kwa mujibu wa Ngure (2003:130);

Methali ni semi fupi zenye maana fiche. Hutumiwa kufafanua ukweli na hekima ya jamii.

Hivyo methali zinapotumiwa, huwa ni semi zinazowatia watu katika hali-ya kutafakari juu ya ukweli fulani. Hupitisha ujumbe kwa undani na kwa maneno machache kuliko lugha ya kawaida. Naye King'ei (1997) anasema kuwa methali hueleza ukweli fulani juu ya maisha ya mwanadamu. Kwa njia ya kimaumbo lakini yenye maana fiche. Hivyo kwa kutumia mafumbo ukweli unawekwa wazi. Kipury 1983:15 anasema ;

Iwapo methali inatumiwa katika mazingira na muktadha unaofaa hupitisha wazo ambalo lingelezwa kwa maneno mengi.

Hivyo basi methali hupitisha maelezo mengi katika mazungumzo yoyote yale. Katika hadithi ya "jitu la kisasa" katika *Pendo la Heba* (1997), methali zimetumiwa ili kuzua ukweli wa mambo .Moja kati ya methali hii ni;

Yaliyopita si ndwele.

(uk. 41)

Methali hii hutumiwa kumaanisha tusingitize yaliyopita, bali hayo yameisha. Tushughulikie na yajayo ambayo yatakuwa na manufaa kuliko yaliyopita. Methali hii imetumiwa kumuhimiza mama, aliyefiwa na mtoto, asahau yaliyopita na ayazingatie yajayo baadaye. Methali nyingine iliyotumiwa kumliwaza mama huyu katika hali yake ilikuwa,

Afadhali mpini kuvunjika badala ya jembe (uk.42)

Methali hii ina maana kuwa mpini ukivunjika bado mkulima atapata mpini mwingine. Jembe likivunjika itakuwa vigumu sana kwa mkulima kupata lingine ili aweze kuendelea na kazi yake. Mpini unalinganishwa na mtoto. Mtoto akifariki, mwingine atazaliwa. Mzazi akifariki, basi huwa ndio mwisho wa mwingine kuzaliwa. Methali hii imetumiwa katika hadithi hii kumhimiza mama huyu kuwa hata ingawa mtoto wake ameaga dunia, mwingine atapatikana maana yeye bado angali anaishi. Methali hii imekusaidia kumpa moyo asihuzunike zaidi bali ajihimize. Hivyo basi methali hii inaeleza ukweli uliopo kwa mafumbo ili kueleza hali ili yote yaeleweke.

Semi hizi zimetumiwa katika hadithi hii ya "Arusi" ili kufafanua ukweli fulani. Katika jamii ya sasa, zimetumiwa kutia ladha kwenye mazungumzo. Methali hutumiwa mara nyingi katika utambaji wa hadithi, nyimbo na hata ushairi simulizi. Hupitisha ujumbe kwa undani

kwa maneno machache kuliko lugha ya kawaida. Methali zimetumiwa ili kutuangazia ukweli wa mambo. Methali hii imetumiwa katika hadithi ya “arusi”, katika chapisho la *Mwendawazimu Na Hadithi Nyingine*.(2000)

subira huvuta heri. (uk. 19)

Baada ya Muriti kumpa Kanana wazo lake kuhusu kuishi pamoja, anatarajia jibu kutoka kwa Kanana. Naye Kanana alipendekeza Muriti asubiri wiki moja. Muriti aliona kuwa wiki moja ni ndefu sana halitakwisha ili aweze kupokea jibu lake. Ndipo basi Kanana alimwambia asubiri ili wiki hiyo ikamilike ndipo aweze kumpa jawabu.

Methali hii ina maana kuwa kusubiri kwa muda, mara kwa mara jawabu lake huwa la heri la kufurahisha na la kuridhisha. Hivyo basi kusubiri kwa Muriti huenda kungemwezesha kupata jawabu ambalo lingemridhisha kutoka kwa Kanana. Baadaye walikuwa marafiki, wakaamua kufanya harusi. Methali nyingine ni ile aliyofikiria Muriti. Anasema hivi

“ Hakuna usiku usiokucha.” (uk. 25)

Methali hii ilitumiwa na Muriti kuonyesha kuwa hakuna kirefu kisichokuwa na ncha au mwisho. Aliitumia kuonyesha hamu aliyokuwa nayo kukutana na rafikiye Kanana. Siku hiyo ilipofika, ndipo alipoona ukweli uliomo katika methali hii.

Katika hadithi ya “Kipara Ngoto”, methali zimetumiwa kueleza ukweli wa hali. Mfano wa methali iliyotumiwa ni:

“Akufukuzaye hakwambii toka.” (uk. 61)

Katika matumizi yake ya kawaida ni kuwa mtu asipokutaka, mara kwa mara, hatakwambia wazi toka. Atatenda kitendo ambacho kitakufukuza mahali alipo. Katika usimulizi, methali hii huambiwa hadhira ili kuwaonya wasiwe wakiingia popote bali wachunge wanaoshirikiana nao. Methali hii pia imetumiwa katika uandishi ili kumwonya Matata kuwa haitajiki katika jamii hii.

Bibiye ami Matata, anapoambiwa Matata atakuja kuishi nao, hakufurahi. Matata alikaribishwa shingo upande na kupokelewa kwa ubaridiubaridi. Haya yalitoshwa kumwonyesha Matata kuwa hakuhitajika mahali hapa. Mwishowe Matata akajiondekea baada ya kumuua mwenzake. Alisema amembandika msimbo wa “Kipara Ngoto”.

Methali hutokea katika maongezi na hurutubisha maongezi ambapo methali zimekuwa zikihifadhiwa kwa kukumbukwa na kuenezwa kimasimulizi. Methali hubeba ujumbe mzito, na hasa wa funzo katika jamii. (Msokile 1992:32) anasema:

maana na hata falsafa katika methali moja ni pana na inabeba uzito wa mawazo yanayoweza kufasiriwa katika vitabu na majarida mbalimbali.

Hivyo basi methali huwa na ujumbe ambao hueleza mengi kuhusu ukweli. Katika hadithi ya “Fumbo la Mwana”, katika kusanyiko la *Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi Nyingine* (2004). Mwalimu Mkuu alitumia methali hii;

“heri kuziba ufa huu tusije tukajenge ukuta (uk 93)”.

Atanasi na mwalimu walikuwa wairekebishe tabia mbaya ya Nanda, kabla tabia ya Nanda kuzidi. Tabia hii mbaya ikiendelea zaidi, bila kurekebisha, itakuwa vigumu kwao kuirekebisha.

Atanansi pia ametumia methali hapo mwisho wa hadithi akisema:

“Akumegeaye tonge humpiga mamako ukitizama” (uk 97)

Methali hii yamaanisha mtu akijifanya mwema kwake akikusaidia, wakati wa shida, siku moja huenda atakutendea maovu. Siku hiyo

hautakuwa na chochote cha kumtendea. Mzee Atanasi anakasirishwa maana anajua mzee Makulu ni rafiki wa kweli. Anamsaidia wakati wa shida. Hata hivyo, alikuwa kampa mtoto wake banki huku hajali maisha yake. Mzee huyu anashangaa hadi akasema :“Makulu, anitende hivi? (uk. 97).

Ana uchungu kwa vile ni rafikiye anamwangamiza.

Methali zilitumiwa kutoa muhtasari wa hadithi yote. Muhtasari wa ujumbe ambao unabainika katika hadithi yoyote ile. Methali ziliibua falsafa ya jamii. Methali hii imetumiwa katika hadithi ya “Ngome ya nafsi” ili kuonyesha Naseko alivyokataa kwenda kwa mumewe. Lakini kama desturi ya jamii, wanawake hawa walisisitiza kuwa hana haja ya kukataa lazima atafika kwa mumewe.

“Ajabu ya shingo kukataa kulala kitandani,” (uk. 101)

Maana ya methali hii ni kuwa shingo likikataa kulala kitandani, basi hayo ni maajabu, lazima likubali kulala kitandani. Naseko alikataa kwenda kwa mume wake kama desturi ya jamii hiyo, wanawake hao walistaajabu.

“Kiingiacho kwa mganga hakitoki babu.” (uk. 101)

Hapo awali, kile mtu alikipeleka kwa mganga hakikutoka kule. Ni malipo ya kazi ambayo mganga amefanya. Kukifikisha kule chochote kile mganga alihitaji, ili aminika miungu walikikubali hivyo basi hakingetoka.

Kwa vile msichana huyu tayari alishashikwa, ni lazima angefikishwa kwa mume wake. Ndipo baadaye kijana wale walimpeleka hadi kwenye nyumba ya mzee Sakaja (uk.102-103). Hadithi nyingine tutakayoichunguza ni ya “Msamaria mwema” ya Ken Walibora. Methali imetumiwa ili kuonyesha jinsi wanyonge hawana nguvu, uwezo dhidi ya wale ambao ni matajari. Likono alisema:

“Hii ni dunia ya dua la kuku halimpati mwewe” (uk 88).

Methali hii imebeba moja kwa moja maudhui ya udhalimu. Udhalimu huu unafanyiwa Likono. Dua ni maombi ya kulaani. Maana ya methali hii ni kwamba kumuapisha na kumlaani mtu anayekushinda kwa cheo, mali au uwezo haina faida. Laana ya mfanyikazi kwa mkubwa wake haina maana kwake. Likono alitumia methali hii kumaanisha kuwa, hana uwezo wa kumfanyia lolote dereva wa gari aliyemfanyia udhalimu huo. Mnyonge atabaki kuumizwa na kuumia chini ya uwezo wa tajiri. Methali ni sifa ambayo hutumiwa katika usimulizi na fanani kusisitiza wazo lake katika usimulizi wake. Sifa hii pia hutumiwa katika uandishi kama jinsi tulivyoshughulikia methali katika hadithi fupi za kisasa. Sifa

hizi jinsi tulivyosema hapo awali hutokea sambamba ili kurutubishana katika kuwasilisha maudhui.

3.3 KUTOTIRIRIKA KWA MAZUNGUMZO

Hali ya kutotiririka kwa mawazo au mazungumzo ni sifa nyingine ya usimulizi. Hali hii huonyesha mshituko wa mhusika, hali ya kawaida ya akili ya binadamu. Katika hadithi ya “ Pendo la Heba”, Musa alipokuwa akilala, alikuwa ndotoni huku alijizungumzia pekee yake . Mazungumzo yake hayakuwa na mtiririko wa moja kwa moja. Kwa mfano, uk.8.

Ati nini?

a-a-a --- a-a-a alisema akajipindua pindua. Utafikiri anajinamizi.

Unasema nini? Lea alimuuliza Musa alipoona kapata fahamu.

Nilikuwa naota niko threatre

Musa alieleza. (uk 8)

Maneno yanamtoka Musa bila mpangilio wowote. Maneno yanayomtoka Musa ni hali ya kawaida ya akili ya binadamu anapoongea. Hali hii ni ya usimulizi ambayo inatumiwa na waandishi katika makala yaliyoandikwa, hivyo kuisitiza kama sifa hizi hutokea pamoja.

3.4 MATUMIZI YA NYIMBO

Nyimbo ni baadhi ya masimulizi ya moja kwa moja (Muriithi 2001). Bakhtin (1981) anaeleza kuwa mwandishi hutumia masimulizi haya ya moja kwa moja katika hata uandishi wa riwaya. Kwa mujibu wa maelezo ya King’ei (1997) nyimbo na mashairi mara kwa mara hutumiwa maana

huwa na athari ya kihisia. Nyimbo hizi na mashairi husisimua na kuvutia hadhira. Nyimbo huimbwa katika usimulizi ili kutoa uchovu kwa wasikilizaji kwa kumsikiliza fanani kwa mda mrefu. Vilevile nyimbo hutumiwa kuisisitiza maudhui ya fanani. Sifa hii pia hutumika katika uandishi. Waandishi wa hadithi fupi hata ndefu hutumia nyimbo ili kuyaweka wazi maudhui yao bila kuwachosha wasomaji wao.

Katika hadithi ya "jitu la kisasa" katika chapisho la *Pendo La Heba* (1997), wimbo umetumiwa kwa ufupi ili kuyaweka wazi maudhui ya hadithi zima. Ujumbe wa kukosa matumaini kuwekwa wazi. Wimbo hutumiwa kuvunja ule mtiririko wa maelezo ya muda mrefu. Wimbo unajitokeza katika ukurasa 40.

Nche nche ncha mumbo nche Nche Nche Mumbo Nchee nche

Kwa kawaida nyimbo ni mbinu ambayo haiwezi kusahaulika na wanajamii kizazi kinavyoendelea kuongezeka. Njogu na Chimera (1999:4) wanasema kuwa;

Kwa vile nyimbo hii aghalabu inamulika maudhui ya hadithi moja kwa moja, basi huwa si rahisi kwa wenye kusikiliza kutokumbuka maudhui

Nyimbo huzua maudhui na kuyaweka wazi ili msikilizaji au msomaji ayaclewe vycina. Wimbo huu ulizua matumaini na kuondoa hofu kwa mama mja mzito.

Wimbo huupia umeendelezwa kwa marefu katika *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000), katika hadithi ya “Jitu la kisasa” ili kuyasisitiza maudhui ya mwandishi. Mwandishi ameuimba wote na kuibua maudhui zaidi ya matumaini.

3.5 URADIDI

Uradidi ni hali ya kurudia jambo au sentensi ili kuisitiza. Wamitila (2002) anasema kuwa katika usimulizi kuna umuhimu wa kutumia uradidi. Vifungu vingi huweza kurudiwa, vingine huweza kubadilishwa kidogo tu. Katika kukisoma kitabu *Kiu cha M.S Mohamed*, tunaiona sifa hii hasa katika sura mbili za mwisho.

Kuna matumizi ya muundo fulani, kwa mfano, ‘miaka mitano’ kukariri miaka aliyoishi Bahati na Idi na ambayo ilikuwa ni ya shida bila raha.

Hadithi ya “Pendo la Heba”. Inayopatikana katika chapisho la *Pendo La Heba*(1997) Musa anapomjibu Daktari kuhusu suala la ndoa, anakariri neno hili “ndoa”. Analirudiarudia ili kuzua uzito na yanayoandamana na asasi ya ndoa. Anasema Hivi :

Hiyo ni ndoa safi sana. Tatizo la vijana kutarajia uzuri katika ndoa. Ndoa ni majukumu. Ndoa ni hasara. Ndoa ni lawama; Ndoa ni kujidunisha na vile vile matusi, raha, kucheka, kukwaruzana. (uk. 4)

Haya ni maneno anayosisitiza kuhusu ndoa, siyo tu kucheka na kuishi katika starehe, bali kutakuwa na kukosana. Katika kuisisitiza mshahara aliopewa daktari siku moja, anarudia “shilingi tatu”.Uradidi huu umetumiwa ili kuisisitiza hoja kama ilivyo katika usimulizi na vivyo vivyo inavyo tumiwa katika uandishi.

“Shilingi tatu, three shillings”. (uk.3)

Kuashiria matatizo yaliyomfikia siku hiyo. Mshahara wake siku hiyo ulikuwa shilingi tatu.Uradidi umetumiwa katika hadithi “ya kisasi” Kwenye *Pendo la Heba* (1997)ili kumpa moyo Njeri.

Onyango anamwambia Njeri uk. 70.

“Usijalil Tulia! tulia! mzigo huu wetu pamoja! Poa! Poal!”

Kurudia maneno haya ni kuisisitiza kuwa Onyango anaelewa hali yake.

Yuko tayari kuwa naye katika shida yake.

Naye Njeri katika ukurasa wa 69 anasema.

Ni wewel Ni wewel
Usikanel Usikanel (uk69).

Maneno haya yanaonyesha uchungu aliokuwa nayo Njeri kuhusu hali yake. Ana uchungu mwingi jinsi vile Onyango alivyomtendea na yuko tayari kulipiza kisasi.

3.6 MONOLOJIA/UZUNGUMZI NAFSIA

Katika mbinu hii, msanii huweka na kuwajenga baadhi ya wahusika, kuwa wanazungumza peke yao na nafsi . Wengi husema huku wakijutia matendo fulani yaliyotendeka maishani mwao. Katika kuzunguka huku sentensi fupi fupi hutumiwa. Maswali ya balagha huenda yatumiwa na mzungumzaji huyu huku akijiuliza, kwa sauti ya chini, kimoyo moyo, au kwa sauti ya juu.

Uzungumzi huu huibua hisia za furaha na uchungu katika maisha ya mhusika huyu. Huibua jinsi anavyoitazama hali yake. Mara nyingine mhusika huyu atarudiarudia wazo kwa mara nyingine kuonyesha umuhimu wa neno hilo. Katika usimulizi sentensi hizi fupi hutumiwa. .

Kwenye hadithi ya “Fumbo la Mwana”, katika *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*(2004).

Mzee Atanasi alijizungumzia mara kwa mara katika hadithi hii.

Nimemlipa shilingi elfu jinsi hii, nikamweleza vizuri tu kuwa zilizosalia nimo katika kusakasaka, mara moja hii kamtia mwana njiani na vibarua pol Alah nkt? Akafyonya :Sasa hivi mvua imeanguka na

tunakimbia kimbia kuandaa konde zetu au tena wakati kushinda barabarani eti kwenda kuwaona walimu? Pol.

(uk. 94)

Anarudia ile Pol Kuonyesha kukerwa na hali ya mwalimu mkuu kumpa mwanawe barua ilhali wakati huo ulikuwa wa kushughulikia hali zingine. Uzungumzi nafsia unamweka mhusika katika hali yake halisi. Msimulizi anapolifikiria jambo lingine katika usimulizi, mara kwa mara yeye huzungumza pekee na baadaye akarejea katika ule usimulizi wake. Hata hivyo huwa ni kuendeleza taharuki miongoni mwa wasikilizaji. Mzee Atanasi anapotoka kwenye ofisi ya Mwalimu Mkuu anazungumza pekee yake.

Akhi! Ana nini mtoto huyu! Ninamteseka na umasikini wote, huu nilionao ale, avae, asome, aje kuwafaa wale wadogo zake watano. Hata mimi mwenyewe asipokuja nifaa kitu. Na jinsi nimpendavyo mpaka mamake asema ninamdekeza, si bure; katundikwa huyu kumbe jirani yangu Andanda hajaacha kuniendea kwa waganga? Akhi! Pol

(uk. 96)

Katika uzungumzi wake, anarudiarudia maneno na milio ya sauti kuonyesha kule kukasirishwa na hali ya mtoto huyu. Usimulizi, utaonyesha wazi mawazo ya msimulizi kwa kiasi, atatoa sauti fulani kuonyesha furaha au kukasirika na mambo fulani katika hadithi yake. Sifa hii hutumiwa ili kurutubisha maelezo ya moja kwa moja kwa kutumia aya.

Katika uzungumzi nafsi mhusika anasemezana na nafsi yake mwenyewe. Hali halisi ya mahusiano yajitokeza wazi. Mukarovsky (1977) anasema kuwa nafsi ya kwanza huwa inajiambia yenyewe au inajisemea kwa nguvu, mpaka watu wanasikia. Naseko anasemezana na nafsi yake, hadi watu wakayasikia mawazo yake. "Ngome ya Nafsi," Naseko anasema;

Mimi niolewe na kikaramba yule! Labda niwe maiti.
Naseko alijisemea moyoni. Lazima nijinusuru kabla
mzee yule kuniharibia maisha.

(uk. 106)

Hivyo, Naseko aliona uchungu kuolewa na mzee huyu rika la babu yake. Alipokuwa akikimbia msituni, huku akitembea alipochoka. Aliambia nafsi yake.

Haidhuru, nitatembea, ni heri kuliwa na mnyama
mwitu kuliko kufungiwa ndani ya ngome ya mzee
Sakaja" Naseko alijipa moyo na kuanza kuchana
mbuga akielekea Mkomani.

(uk.109)

Mazungumzo haya nafsia yanaibua hisia moja kwa moja ya mazugumzaji yanayoonyesha machungu yake anapopigana na hali yake inayomsonga. Sifa hii imetumiwa kurutubisha maandishi hata ingawa kimsingi ni sifa ya usimulizi.

3.7 MATUMIZI YA KUCHANGANYA NDIMI

Sheng hutumiwa miongoni mwa vijana hasa wa mitaani. Huwa ni mchanganyiko wa Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zingine. Katika Hadithi ya "Kipara Ngoto", Matata anaitumia lugha hii kuonyesha kuwa alikuwa mtoto aliyelelewa mtaani. Lugha hii hutumiwa miongoni mwa vijana kwa minajili ya kuwaficha wazee wasijue yale wanayoyazungumzia. Matata anatumia maneno kama vile;

Mazee! Huyu **dem ni msoo jo** (uk 64) kumaanisha msichana yule ni mkubwa.

"Kuna **ziki fit** kwenye **mathri ile**". Matata anasema hivi kumaanisha kuna muziki mtamu katika gari lilo la abiria.

"Nikimpata aliyenibandika hiyo **name jo** atanitambua **just wait.**"

uk. 64.

Matata ametumia lugha zote mbili. Kiingereza na Kiswahili. Hali hii yaonyesha kuwa, hakimudu Kiingereza vizuri na pia Kiswahili vizuri. Anamaanisha yule atakayempata kuwa ndiye aliyemandika msimbo huo basi, atapata adhabu kali.

Yule dem brown uk. 65
wendapi mazee?
wee nisare jo

Sentensi hizi zote zaonyesha hali ya maisha yake ilikuwa imeharibika.

Ametumia pia Kiingereza hiki kuonyesha kiwango cha elimu yake.

Katika mazungumzo kati yake na ami yake anasema;

I am sorry uncle (uk. 62)

Matata anaungama makosa yake ya kusoma kwa sauti kitabu chake cha

“Hardly Chase.” (uk. 62)

Anapomweleza, binamuye kuhusu maisha yake ya shuleni, anamwambia kwamba alifukuzwa shule tatu. Anatumia maneno ya Kiingereza kama.

Tereni **secondary**

Koelel **high school**: (uk. 63)

Alikuwa **ring leader**

Matumizi haya ya Kiingereza yanaonyesha kiwango chake cha elimu. Sifa hii mara kwa mara huonyesha hali na hadhi ya mazungumzo yoyote. Sifa ya kuchanganya ndimi hutumiwa katika mawasiliano, katika maandishi au hata katika mazungumzo. Sifa hii imetumiwa katika hadithi hii ya “Msamaria Mwema” ikijitokeza katika mazungumzo na fikra za binadamu.

“Likono aliyefanya kazi ya utarish
katika maktaba ya Government press”

(uk. 79)

Chumba hiki kinajulikana sana mjini hivyo, tutaelewa kuwa, mtu huyu alifanya kazi mjini. Wale waumini wanapomsaidia Likono baada ya ajali,

mwenye gari alikuwa na shughuli ya simu yake. Wao walisema;

“Mwangalief Mobile ndiyo muhimu” (uk. 80)

Walikerwa na jinsi mwenye gari alichukua simu ya mkono kuwa ya muhimu kuliko uhai wa binadamu.

Mwenye gari alipokuwa akiwasiliana na mwenzake kupitia kwenye simu alisema;

“Fanya hivi njoo Giftel Hospitla mara moja --- eh emergency”
(uk. 86).

Sentensi hii ina maana ya jambo la dharura. Dereva wa gari hilo hilo alipoombwa atoc pesa ili mgonjwa akafanyiwe upasuaji, alisema hakuwa na pesa bali alikuwa na “Euro Card”. Dereva yule hakuwa mtu wa hadhi ya chini wa kubeba pesa bali kubeba “Euro Card” atakayotumiwa kupata pesa kwenye benki. Kubadilisha ndimi hujitokeza katika mazungumzo, ili kumfanya msomaji kuelewa yanayo zungumzwa.

3.8 HITIMISHO

Tumeshughulikia sifa za usimulizi katika sura hii. Tumetoa ufafanuzi huku tukitoa mifano ya hadithi katika machapisho ya Hadithi fupi ya hivi karibuni. *Pendo la Heba* (1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine cha* (2000) wa *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Mazungumzo yametumiwa ili kuibua hisia za wahusika moja kwa moja. Kuchanganya ndimi ni sifa iliyotumiwa ili kuonyesha ni watu wa aina

gani wanaozungumza. Katika hadithi kadhaa uzungumzi nafsi, umetumiwa ili kuonyesha mvutano walio nao. Sifa hii huzua zaidi mvutano wa muhusika na nafsi yake na baadaye akasema kwa sauti anayoyafikiri. Sifa zingine kama vile nyimbo, methali, uradidi na kutotiririka kwa mazungumzo, zimetumiwa ili kusisitiza usimulizi katika hadithi fupi za kisasa.

Sifa hizi zimetumiwa na mwandishi ili kusisitiza maudhui yake na pia kupunguza uchovu wa kusoma aya kila wakati. Sifa hizi za usimulizi zimetumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili ili kuendeleza wazo la umuhimu wa sifa hii katika fasihi ya Kiswahili. Sifa hizi hurutubisha na kuchangia sifa zingine za hadithi fupi. Tutaangazia pia sifa za uandishi ambazo zimetumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Tutaziweka wazi huku tukitoa mifano katika hadithi fupi za Kiswahili. Tutashughulikia pia sifa kama matumizi ya aya, barua na upenyezi wa mwandishi kama za uandishi na hata pia jinsi zinavyotumika katika usimulizi.

SURA YA NNE

4.0 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita tumchangazia mbinu ya usimulizi na sifa kadhaa za usimulizi. Sifa hizi ni kama vile mazungumzo, methali, nyimbo na jinsi zimebainika na kutumiwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Ingawa sifa hizo zinahusishwa zaidi na usimulizi, zinapatikana pia katika uandishi. Hali hii inaonyesha kwamba kuna mwingiliano kati ya sifa za usimulizi na uandishi.

Katika sura hii tutaangazia mbinu ya uandishi. Tutazingatia uandishi kama mbinu moja wapo inayorutubisha usimulizi ili kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Ili mwandishi aweze kueleza maudhui yake kwa ufasaha, atahitaji kujishughulisha na uandishi na sifa zake ambazo zitayaweka maudhui wazi bila kumkanganya msomaji au msikilizaji.

Uandishi ni mbinu ambayo hueleza kwa njia ya kutumia maneno yasiyobadilika, maneno yaliyoandikwa huwa yale yale. Mbinu hii, hutegemea vipengele vya kiisimu ambavyo mwandishi atachagua katika uandishi wake.

kuvitumia ili kufanikisha ujumbe wake.(Ong 1982:39) anasema:

Katika uandishi, hali ya mawazo yasiyohitajika
huwa hayatumiwi, bali yanatupiliwa mbali.

Kulingana na mawazo ya Ong si kweli kwamba yasiyohitajika katika uandishi hutupiliwa mbali. Waandishi huenda wakatumia uradidi katika ushairi ili kuisisitiza wazo fulani. Katika uandishi mwandishi huzingatia yale atakayo kuyashughulikia kwa ufupi. Waandishi wengi huenda wasikaribie maisha ya kawaida kama ilivyo katika usimulizi. Wao huzingatia mambo ambayo ni ya kidhahania kuliko katika usimulizi. Wao huzingatia miongozo ya kufanya jambo fulani, katika uandishi wao. Hata hivyo waandishi na wasimulizi wote hujaribu kukaribia maisha ya binadamu kupitia ubunifu wao.

Uandishi huzingatia ukamilifu wa matini, sentensi ambazo zimekamilika na ambazo hazitazua utata akilini mwa wasomaji. Mwandishi huzingatia utaratibu fulani katika kueleza maudhui yaliyokusudiwa. Iwapo sheria za kiisimu hazitafuatwa na mwandishi, basi itakuwa ni kuvuruga kule kuelewa ujumbe wa mwandishi kwa msomaji.

Katika sura hii, tutashughulikia sifa za uandishi. Tutaangazia sifa hizi huku, tukitoa mifano kutoka kwa machapisho ya hadithi fupi tuliyoteua.

Tutazingatia mifano ya hadithi katika *Pendo la Heba*(1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*(2003) pamoja na *Mayai Waziri wa maradhi na Hadithi zingine*(2004).

Tutaangazia mifano ya sifa hizi na jinsi zimetumika katika hadithi hizi fupi.

4.1 MAELEZO KATIKA AYA

Maelezo ni sifa moja ambayo imejitokeza katika hadithi fupi. Sifa hii ni mojawapo ya sifa za uandishi. Mwandishi hueleza moja kwa moja hali ya mhusika, na kueleza hali yake, na yale anayoyapitia na mawazo yake kuhusu mambo fulani. Mawazo ya mwandishi yametiririka na ametumia sentensi ambazo zimekamilika.

Kando na hayo, mwandishi ametumia sarufi sanifu ili kuelezea mawazo yake kuhusu wahusika hawa ili iweze kukamilika. Mwanzo kabisa, tunaelewa hali ya Musa katika hadithi ya “Pendo la Heba” na jinsi alivyokuwa akifikiri sana. Maelezo ya jinsi alivyovalia yalisisitizwa na vile alivyofunga saa mkononi na ambayo mkanda wake ulikuwa umesaki. Maelezo ya sebuleni kwake yanatolewa ili tufahamu jinsi sebule hiyo ilivyoundwa. Baada ya maelezo haya kuhusu Musa na jinsi nyumba yake iliyokaa, ndipo alishtuliwa na pesa kuwa simu ilikuwa inalia.

Baada ya maelezo, baadaye kulizuka mazungumzo ya simu. Baadaye pia kulikuwa na maelezo juu ya shida zilizotokea katika nyumba hiyo. Baada ya mazungumzo mwandishi anaeleza juu ya wahusika, hali yao na mazingira yao. Anatumia sentensi zilizokamilika ili ujumbe wake ueleweke na msomaji. Maelezo hayapatikani katika uandishi pekee. Maoni yetu ni kwamba maelezo hutumiwa pia katika usimulizi. Msimulizi huenda akaeleza juu ya safari ya majitu, jinsi walivyosafiri na baadaye wakafika. Msimulizi huelezea jinsi mhusika fulani alivyokimbia ili aepukane na hatari fulani. Maoni haya ni kususitiza kuwa mbinu hizi huenda sambamba.

Wafula ambaye ni Mwandishi wa hadithi ya "jitu la kisasa" katika chapisho la *Pendo la Heba* (1997) ametumia maelezo ya moja kwa moja ili kuelezea hali ya maneno. Anaeleza juu ya matanga yaliyotokea katika kijiji hiki cha Lambaka kwa mzee Lomo. Hivyo basi anatupatia picha ya yale yaliyotukia katika kijiji hiki kwa mtiririko wa moja kwa moja. Anatumia sentensi zilizokamilika ili kuweza kuufanya ujumbe wake ueleweke. Anapoeleza kuhusu matanga haya anasema;

Hivi majuzi matanga yalifanyika katika kijiji cha Lambaka nyumbani mwa mzee Lomo. Mtoto wake wa kike alivamiwa na ugonjwa wa ghafla, akabebwa hobelahobela hadi kwenye kituo cha matibabu huko Gululu. Madaktari na wahudumu wengine wa hospitali hiyo walifanya kila juhudi kumrudishia msichana huyo nafuu. Jitihada zao hazikufua dafu, hawakuweza kuondoa kudura.

(uk. 10)

Katika maelezo haya tunaelewa kuwa mtoto huyu alikuwa anaogua sana na akapelekwa kwenye hospitali ili apate matibabu. Maelezo yametumika kuweka wazi yaliyoyokea na yanatiririka ifaayo. Sifa hii ya maelezo ni ya uandishi ambayo inaeleza mawazo mengine bali mawazo yanaelezwa ili yaeleweke vyema na wasomaji.

Maelezo hutumiwa na waandishi ili kuweka wazi maudhui kwa ufupi. Huelezwa mambo yasiyojulikana kwa msomaji na kuyaweka wazi. Aya ndefu za maelezo zimetumiwa kama sifa moja ya uandishi. Sentensi zilizokamilika hutumika huku mawazo yakitiririka kwa ufupi, tofauti na uzungumzaji mwandishi anapotumia maelezo katika kazi yake, yeye huwa na nafasi ya kubainisha chuki au mapenzi dhidi ya wahusika wake. Hata hivyo msimulizi atayatumia maelezo kuendeleza maudhui yake. Ataeleza safari fulani au tukio katika hadithi hiyo. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mbinu hii humpa msomaji fursa ya kutathmini mhusika fulani. Msomaji analazimika kuukubali msimamo, na kuridhika na maelezo ya mwandishi.

Katika hadithi ya “Korti ya Kishenzi”, kwenye *Mwendawazimu na hadithi Nyingine* (2000) katika aya inayozungumzia mapenzi kati ya Ngoloso na Faith, tunatambua sifa za Ngoloso na Faith katika mapenzi yao.

Tangu mapenzi baina ya Faith na Ngoloso yaanze, mwanamke huyu alijihisi kwamba, aliyokuwa akifanya siyo sawa. Lakini angefanyaje na Ngoloso alikuwa “Bosi wake” mbali na hayo, ngoloso alikuwa na sifa chungu zima zilizowafanya wanawake wengi kuvutiwa naye. Alikuwa na umbo la kuvutia sana, na alifahamu vizuri mizungu yote ya kutongoza na kubembeleza mapenzi. Halafu ukarimu wake ulikuwa hauna kifani. Tayari Faith alikuwa amefaidika sana kwa zawadi ghali na nyingi alizopewa na Ngoloso; tangu televisheni ya rangi hadi mazulia, ya kutoka nje ya nchi . Kwa kifupi Faith alihisi kwa kuwa hana uwezo wa kujibandua kutoka kwa Ngoloso (uk 32)

Kutokana na maelezo haya, tunatambua kuwa Faith hana uwezo hata wa kujibandua kutoka kwa mtego aliojitia. Maelezo haya yanampa msomaji fursa ya kumhurumia Faith. Vivyo hivyo maandishi haya yanaonyesha mtazamo alionao mwandishi kuwahusu Faith na Ngoloso.

Sifa hii imempa fursa mwandishi wa hadithi hii kusema mengi kuwahusu wahusika na matukio kwa ufupi. Aya zingine zimetumiwa kuelezea matukio kadhaa katika hadithi hii. Aya inayoelezea hali ya Agnes inatuelekeza kumfahamu Agnes Zaidi(Uk 28).

Maelezo yametumiwa ili kuelezea yale yaliyotukia wakati huo. Ametumia sentensi zilizokamilika ili kufanikisha uelewaji wa ujumbe wake. Aya hizi

zina muumano na muwala unaozifanya kueleweka, Wamitila (2002) .
 Vijischemu vya aya hizi vimepatana vilivyo ili kuwasilisha ujumbe.
 Vijischemu ambavyo havihitajiki vimetupiliwa mbali.

Hadithi ya "Arusi", kwenye *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*_(2000)
 mwandishi anaeleza kuhusu harusi ya Kibwi na Kathure. Anatuelekeza
 jinsi mambo yalivyokuwa katika harusi hiyo. Mwandishi ametumia
 mbinu hii ili kuweka wazi yale yaliyotendeka . Anatumia maelezo haya ili
 kuiweka wazi picha ya wahusika pamoja na dhima zao. Mwandishi
 anasema:

Baadaye maharusi walikata keki, kama kielelezo cha
 jinsi wataleana na kutunzana katika maisha yao ya
 ndoa. Kitendo hiki kilishangiliwa sana na watu.
 Kitendo hiki pia ndicho kilichofunua masufuria
 makubwa ya wali na vyakula vinginevyo kwa sababu
 baada ya hapo ndipo chakula kilipakuliwa na mlo
 ukaanza kwa kila mtu. Nao ulikuwa mlo wa
 kutajika. Vinywaji vya baridi kama vile soda na maji
 ya matunda zilifurika watu wakaogelea kwavyo.

(uk.14)

Maelezo haya yanatupa picha halisi vile Arusi hiyo ilivyoendelea na kuwa
 ya kufana. Ametumia mbinu hii ili kuyaeleza matukio na kutoa hata
 maoni kuhusu wahusika wake.

Aya nyingine imetumiwa katika hadithi ile ile ya “Arusi” baada ya gurudumu la gari kupasuka;

Mayowe ya uchungu , kimako na simanzi yaliipapwa anga, na kuangamiza kabisa utulivu wa furaha uliojaa nyoyoni za watu. Kundi la wanaume liliteremka bondeni kuifuata gari iliyokuwa si gari tena, bali ni kidude cha chuma .Walimkuta Kanana amezirai, lakini mwili wake ulikuwa kama ulivyokuwa kabla ya tukio hilo, hajakwaruzwa pahala. Murithi alikuwa amesagwa kabisa kiwiliwili chake kimevunjika, na kichwa chake hakionekani walimwosha Kanana, wakamlaza chini ya kivuli cha mti. Wakawa wanampepea kwa matawi mpaka akazindukana, Wengine waliendelea kukitafuta kichwa cha Muriti.(uk 27).

Hali hii ilikuwa ya uchungu na ya kuhuzunisha. Hali hii ilizua hali ya taharuki akilini mwa wale waliohudhuria harusi hii. Maelezo haya ni ya uandishi ambayo mwandishi wa fasihi mara kwa mara huenda asikwepe kutumia. Hutumia ili kurutubisha kazi yake ya fasihi. Mwandishi anaweza kueleza kwa ufupi mambo mengi yaliyotokea, ili msomaji aweze kuelewa kwa kifupi yote yaliyotokea.Ujuzi huu wa kueleza mambo kwa ufupi hurutubisha usimulizi kwa kutoa maelezo haya kwa wasikilizaji ili kuelewa zaidi maudhui.

Sentensi ambazo zimekamilika zimetumika ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Mshikamano na muwala unajitokeza katika sentensi hizi na jinsi zinavyofuatana. Mshikamano kwa mujibu wa Halliday na Hassan

(1976) huwa ni dhana ya kisemantiki inayoelezea uhusiano wa kimaana unaopatikana katika matini. Uhusiano huu umejitokeza katika aya alizotumia mwandishi. Muundo umejitokeza kutoka kwa sentensi moja kwa hadi nyingine, kutoka kwa aya moja hadithi nyingine. Beargrande na Dressler (1981:84) wanasema;

Muwala umefungamanisha na jinsi maana inavyoweza kutumiwa kudhihirisha uwezo wa lugha. Sentensi hii inahusiana kimaana ili kukamilisha ujumbe.

Neyole (2003;43) anasisitiza kuwa muwala hutokea kunapokuwa na mwingiliano na uthabiti katika mwendelezo wa hoja na utambuzi. Jambo hili linatokea katika hadithi ya "Kipara Ngoto" katika *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000). Maelezo kadha katika aya yametumiwa ili kuwasilisha maelezo mengi kwa ufupi. Sentensi hizi zimepangwa kwa mtiririko wa lugha kimaantiki. Zimetumiwa kuwasilisha maoni ya mwandishi kuhusu wahusika, hali yao na hisia zao. Basi baba alipomdokezea mama kuwa Matata ataishi nao, mama hakufurahia wazo hilo:

Mama alikeketeka kwa tangazo hilo, ndilo lilonifanya nigundue kuwa kakerwa, ni vita baridi alivyovipiga baba siku nyingi baada ya tangazo hilo. Mama alijiinamia kama kondoo. Alipoulizwa lolote na baba, jibu lake lilikuwa jicho la hasama tu, ungedhani kazaliwa bubu tangu hapo pamoja na umri wangu mdogo nilibaini pamepita hitilafu katika mahusiano ya wazazi wangu. Kisa na maana hitilafu hiyo, ni Matata, binamu yangu mjalaana. Wazo hilo liliamsha

chuki moyoni mwangu. Nikamchukia matata ukomo wa kuchukia hata kabla hajawasili kwetu nikamtia macho.

(uk. 61)

Aya hii ina mtiririko wa mawazo kutoka sentensi ya kwanza hadi ya mwisho. Sifa hii ya uandishi huweza kutumiwa ili kufafanua zaidi kuhusu wahusika na hali yao. Mama alikerwa na wazo la baba. Hakufurahia maoni yake, na kwa hivyo alinyamaza kimya, na huku amekarisirishwa na wazo hilo. Mwandishi ametumia maelezo haya ili kutathimini hali na mvutano wa ndani uliokuwepo kati ya wahusika.

Aya zingine zimetumiwa sambaba na sifa za usimulizi. Zimetumiwa kutoa maelezo marefu kwa kifupi ili kuisitiza mawazo ya msimulizi. Maelezo hutumiwa na msimulizi ili kuelezea hali ya wahusika wake na safari zao na kufanya hivyo kurutubisha masimulizi.

Maelezo yametumiwa ili kufafanua zaidi hali ya mhusika na yote aliyoyapitia kwa ufupi. Mengi huenda yalimtendekea mhusika, lakini mwandishi huchukua fursa kuelezea huku akifafanua kwa kutathmini mhusika kwa ufupi. Kutumia sentensi zilizokamilika, sarufi, uakifishaji wake ili kuwasilisha ujumbe wake kwa ufupi. Kupitia kwa maelezo ya aya mwandishi, hupenyeza akatoa maoni yake. Mwandishi anaweza kujitokeza kwa njia kadhaa katika uandishi wake. Mwandishi anaweza

kusema mambo fulani, kuhakiki, kutathmini kutoa hoja zake anazofikiri, na baadaye kuhitimisha kwa maoni yake kuhusu hali hiyo au mazingira ya wahusika (Wamitila 2002).

Katika kufafanua hoja yake mwandishi humwelekeza yule msomaji, kwenye mtazamo fulani. Msomaji hapewi fursa ya kumhukumu yule mhusika. Katika hadithi hii ya “Ngome ya nafsi” kwa mara mwandishi ametumia maelezo kufafanua hali ya Naseko na mazingira yake.

Kufumba na kufumbua, Naseko aliibwaga ndoo ya maji chini kwa kishindo, huku maji yakiwamwagikia vijana hao. Alijipenyeza kati yao kama risasi na kufyetuka kuelekea kwao. Hakuweza kupiga mayowe kwa hofu kuu iliyomvaa akabaki akihema na kupumua huku vijana wale wakiwa mbio nyuma yake. Hakufika mbali walimvaa mzima mzima na kumbeba juu mzegamzega. Naseko alitoa unyende mkali uliozimwa mara moja na kofi kali lilitoka kwa Mbanda, kijana mwenye kiburi na wingi wa mshauo.
(uk 100).

Hali ya Naseko ilikuwa ngumu kutokana na maelezo haya. Hangeweza kujinasua kutoka kwa mtego huo, wa kuozwa kwa mume aliye sawa na rika la babake. Maelezo haya yanaweka wazi hali ya Naseko na hofu yake kuhusu maisha yake. Mwandishi ametumia maelezo mengi kuelezea hali ya mzee Sakaja, na mke wake (uk. 104).

Aya ya mwisho ya hadithi inaonyesha jinsi Naseko anapata pumziko baada ya kupigana na hali yake ngumu. Hali ya kukabiliana na vijana waliomlazimisha kuolewa na mzee aliyekuwa rika la babake.

Baada ya shughuli za siku, Naseko alijipumzisha kitandani mwake. Aliwaza juu ya kisa chote cha kutoroshwa kwake na kukiona kama jinamizi. Aliwaza juu ya wale wasichana kama yeye ambao hawakubahatika kutoroka kama yeye. Aliwaona kama viumbe waliofungiwa ndani ya ngome za nafsi zao wenyewe (uk. 114).

Maelezo mengi yametumiwa kuelezea hali tofauti kwenye hadithi ya "Msamaria Mwema" inayopatikana katika chapisho la *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Mwandishi ametumia maelezo haya ili kufafanua na kutoa maoni yake kuhusu hali za wahusika wake. Ametumia maelezo kwa urefu na kupuuza mbinu zingine za usimulizi. Mwanzo kabisa anaeleza jinsi siku ya Likono ilivyoanza:

Jumapili siku ambayo Likono aliamini alishiba matumaini na uzao upya wa maisha yake kama binadamu. Jua lilikuwa ndio linajitahidi kutokeza nyuma ya mawingu yaliyotanda angani lilifanya hivi kwa hadhari kama mtoto asiyejua afanye jambo alilokatazwa au la. Mvua nyepesi iliyonyesha jana iliacha vidimbwi vya maji madafu hapa na pale, kando ya barabara za jiji la Nairobi.

(uk 78).

Maelezo haya yanafafanua, jinsi siku hiyo ilivyokuwa. Haikuwa ya matumaini sana kwa Likono hata ingawa yeye alikuwa kaamini kushiba matumaini na uzao mpya wa maisha yake kama binadamu. Maelezo haya hutokea katika usimulizi. Fanani hueleza matukio fulani, matatizo yaliyomfikia na suluhisho lake.

Mwandishi ametumia maelezo mengine marefu (77-80) kuelezea jinsi mambo yalivyomwendea mrama Likono. Mengine kutoka (81-82, 85, 88) yanayoelezea kuhusu hali ya Likono, alivyopata matibabu na baadaye msamaria mwema, kutoroka jukumu lake la kumtibu Likoni baada ya kumgonga na gari lake.

Maelezo haya, yanamfanya msomaji ayachukulie yale aliyoyaeleza mwandishi kama kweli. Hana fursa ya kutoa hatima yake kuhusu aliyoyasema mwandishi. Mbinu hii hutokea katika usimulizi. Maelezo ya ziada husimuliwa ili mhusika aweze kuyaelewa maudhui ya msimulizi.

4.2 MATUMIZI YA BARUA

Barua ni mawasiliano baina ya watu wawili au zaidi kwa maandishi. Hutumiwa kuarifu, kuuliza jambo au kuhakikisha jambo fulani (Muriithi 2002:63).

Barua ya kirafiki husimulia mambo ya kindani baina ya wahusika. Katika hadithi ya "Korti ya Kishenzi", Kanu alimwandikia Faith barua ili kuwasilisha ujumbe wake wa ndani kwa Faith. Ujumbe wake hasa ulikuwa wa kumuonya Faith aachane na bwanake na akatafute mume mwingine atakayemwoa. Kanu anasema katika barua yake kuwa:

Kwa Faith binti Kasimbi,

Jina langu ni Agnes Kanu, bibiye Onesmas Ngoloso, Bosi wako. Nakuandikia ili nikufahamishe kuwa najua uhusiano uliopo baina yako na mume wangu. Wewe ni mwanamke uliyesoma na uliye wa kazi nzuri. Tena ni mwanamke kijana mrembo. Kama unataka mwanamume wa kukuoa au wa kufanya mapenzi naye, unaweza kupata kwa urahisi.

Tena siyo mmoja au wawili ni wengi kiasi utakacho. Kwa nini usitafute; vijana badala ya kunyakua wanaume za watu? Uchungu nilio nao rohoni kuhusu matendo yako maovu ni mwingi sana. Hata hivyo, Hata hivyo najizuia kuwasiliana nawe kupitia kwa matusi. Tafadhali achakutembea na mume wangu.

Mimi wako,
Agnes Kanu Ngoloso(uk.31-32).

Barua hii inasawiri machungu aliyokuwa nayo Agnes. Sifa hii ni ya uandishi inayotumiwa ili kuwasilisha ujumbe wa kirafiki. Inaelezea hisia za ndani za Kanu kumhusu Faith.

Barua huwasilisha mawazo ya ndani ya mtu, hasa ya kirafiki. Muriithi (2002). Katika hadithi ya "arusi Kibwi" anamwandikia rafikiye Muriti barua ili kumweleza mawazo yake ya ndani kuhusu uhusiano wake na

Kanana. Anamweleza wazi hali ya msichana huyu, ukoo wake, na jinsi ambayo ingekuwa bora kama hangemuoa msichana huyo hutoka kwa jamii ambayo wasichana hawaoleki. Mawaidha haya yalimsumbua Muriti kwa vile yeye alikuwa kaamua kumuoa.

Kutokana na barua hii, msomaji anaweza kuelewa kuwa Kibwi hakupendelea Muriti amwoe Kanana. Hivyo kumuacha msomaji katika hali ya taharuki vile Muriti angesuluhisha tatizo hili.

Barua hii inafafanua wazi jamii anamotoka Kanana, kama sababu thabiti ya kutoolewa na Muriti. Barua hii inatoa maelezo marefu kwa ufupi, kuhusu hisia za Kibwi kuhusu ndoa ya Kanana na Muriti. Msimulizi hutoa hisia zake kwa kuimba au kutoa mlio wa mnyama, kutumia uso wake ili kuwasilia hisia fulani. Barua hurutubisha usimulizi kwa vile hutumiwa kuwasilisha ujumbe kwa nchi za mbali. Barua hutumiwa na msimulizi anapoelezea hadithi ambayo mhusika alienda nchi za mbali, hivyo basi ujumbe kwa kutumia barua lazima upelekwe. Sifa hii hurutubisha usimulizi kwa kuibua maudhui zaidi ya msimulizi.

4.3 UPENYEZI WA MWANDISHI

Mwandishi anaweza kujitokeza kwa njia ya kuyasema mambo anayofikiri, anayotajia yatendeke au kuhakiki. Wamitila (2002:48) anasema;

Mwandishi anaweza kujitokeza kwa njia ya wazi kuyasema mambo fulani, kuhakiki na kutathamini kutoa hoja, zake, maoni yake.”

(uk. 48)

Mwandishi anaweza kuyasema ili kufichua yale yaliyoachwa anayofikiri juu ya wahusika, hali na matukio katika hadithi hiyo . Atasema haya ili kufafanua matukio ili yaeleweke. Wamitila anatoa mfano kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974). Mwandishi anatoa hukumu na maoni kuhusu kitendo cha kazimoto cha kujua.

Katika hadithi hii ya Jitu La kisasa, iliyomo katika chapisho la *Pendo la Heba* (1997) mwandishi anafafanua zaidi kuhusu mama aliyeingia na asiyejulikana na watu wote:

Mwendo wa saa mbili unusu za usiku hivi, mama mmoja alifika. Pamoja na kuvaa rinda lililomkaa vizuri, alikuwa amejifunga kanga kiunoni, miguuni alikuwa na sandali zisizoweza kufahamika bayana kuwa kama ni za kiume au ni za kike. Kichwa chake kilikuwa kimefunikwa na kitambaa cheupe. Schemu ya kitambaa ilienea chini na kufunika pande zote mbili za mashavu.

Ajabu nyingine ilikuwa kwamba huyu mama hakuonyesha uso wake-wazi. Hajulikani kule alikotoka, lakini hapakuwa na haja ya kujua

alikutoka. Hata wapita njia waweza kuhudhuria matanga bila kushukiwa kwa lolote.

“Naam, nani mkosa shukrani asiyeweza kubaini nia njema katika kitendo kama hiki?”

(uk 68)

Maelezo haya yanaashiria ufafanuzi wa mwandishi, na baadaye kuhakiki na kutathmini hali ya mama huyu. Anatoa maoni yake kuhusu mama huyu kwa vile ambavyo hakujulikana. Katika kuyatoa maoni haya, anamuelekeza msomaji katika njia fulani ya kuusawiri ulimwengu kwa kupitia maoni yake. Mwandishi anatathmini maisha ya Njeri katika hadithi ya “Kisasi”, baada ya yeye kujipata na hali hii. Anatoa maoni yake na kuhakiki hali ya Njeri. Anasema;

Tangu siku hiyo Njeri alifungua ukurasa mpya katika maisha yake. Hapo mbeleni alikuwa msichana ambaye alijjali kwa kila hali. Alijali mavazi yake, alijali masomo yake na uhusiano wake na watu ulikuwa mwema. Kuanzia siku hiyo, Njeri hakujali kama alikuwa amechana nywele zake ama la. Hakujali jinsi alivyovaa wala kama alifanya kazi ya darasani. Isitoshe, alianza kunywa pombe na kuchukuliwa na mwanaume yeyote aliyeonyesha dalili ya kumpenda.

(uk. 34)

Haya mawazo ya mwandishi yametufanya tuelewe hasa hali ya Njeri baada ya kujua kuwa ana ugonjwa huu. Hamini na kujielewa bali anapoteza matumaini maishani.

Upenyenzi wa mwandishi ni sifa inayojitokeza katika usimulizi. Msimulizi huongezea mawazo yake huku akitathmini mhusika fulani. Yeye huongeza maneno ya ziada ili kumfanya msikilizaji afikirie zaidi. Mbinu hizi basi hutokoa pamoja. Mbinu hizi huchangiana na kurutubishana.

4.4 HITIMISHO

Uandishi ni sifa inayotumiwa na waandishi kuweka wazi maudhui. Jinsi jamii inayoendelea kukua na kuendelea ndivyo pia maudhui yanavyobadilika. Tumeangazia jinsi sifa za uandishi zilivyotumiwa katika hadithi hizi. Waandishi wametumiwa sifa za uandishi kwa ufundi wa hali ya juu ili kudhihirisha maudhui katika jamii ya sasa. Maelezo katika aya ni sifa iliyotumiwa katika hadithi fupi tulizochunguza. Aya katika hadithi hizi zimezingatia mtiririko wa sentensi na hata ujumbe. Aya hizi zimezingatia mshikamano na muwala ili kueleza ujumbe katika hadithi hizi. Barua zimetumiwa ili kuwasilisha ujumbe wa ndani kwa wahusika. Barua zilizotumika zilikuwa barua za kirafiki. Kuzingatia upenyenzi wa mwandishi, amewatathmini wahusika wake, na kufafanua zaidi hali yao kulingana na maoni yao. Upenyenzi huu, humfanya msomaji, ayakubali maoni ya mwandishi, bila kutoa maoni yake kuhusu wahusika hawa.

Uandishi umeweka wazi maudhui kwa ufupi, ili kumdokezea msomaji ujumbe huu kwa ufupi bila kuongezea yale yasiyohitajika. Hata hivyo maudhui yalizingatia na kuwekwa wazi ili yafahamike wazi.

Kwa kuzingatia maoni yetu, mbinu hizi hutumiwa kwa pamoja ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi au msimulizi. Sifa hizi tulizozishughulikia hutumiwa katika usimulizi na uandishi jinsi tulivyoelezea. Msimulizi anaweza kuyaeleza matukio fulani ya wahusika au sherehe fulani huku akibadilishana na nyimbo, methali au maelezo mengine.

Mwandishi anaweza kutumia upenyezi huu akieleza na kutathmini wahusika katika jamii wanaofanana na wale aliowatumia katika usimulizi wake. Sifa hii hutumiwa kurutubisha usimulizi hata ingawa sifa hii imechukuliwa kuwa ya uandishi. Barua ni sifa nyingine inayotumiwa katika usimulizi kupeleka ujumbe kwa watu au mtu anayeishi mbali. Sifa hizi hurutubishana na hakuna sifa inayojisimamia ili kuwasilisha maudhui. Katika sura inayofuata tutaangazia hitimisho na matokeo ya utafiti wetu. Tutatoa mapendekezo yetu kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wetu.

SURA YA TANO

5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tashughulikia hitimisho la utafiti huu kwa jumla, matokeo ya utafiti huu na mapendekezo kutokana na matokeo ya utafiti huu. Tutaangazia hitimisho la sifa za usimulizi na uandishi na jinsi zilivyoingiana kwa ufupi. Tutaonyesha matokeo ya utafiti huu na mwisho tutatoa mapendekezo kulingana na utafiti huu.

5.1 HITIMISHO NA MATOKEO YA UTAFITI

Tasnifu hii ililenga kuchunguza umahuluti katika hadithi fupi za Kiswahili. Lengo letu pia lilikuwa ni kuchunguza jinsi umahuluti huu unajitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Umahulutu ni dhana ambayo ina maana ya utamaduni unaoibuka kwa kuchanganya tamaduni mbili au zaidi. Nilishawishika kushughulikia mada hii kwa sababu ya jinsi hadithi fupi za sasa za Kiswahili zimetumiwa kuwasilisha maudhui ya sasa hivi.

Mwanzao wa kinyakani kuhusu utanzu huu kuma ni mwendelezo wa

kistari wa ngano, mawazo haya yalinitia mshawasha wa kufanya utafiti ambao ni tofauti.

Utafiti huu unatofautiana na ule wa awali kwa vile umeshughulikia umahuluti unaojitokeza katika hadithi fupi za kisasa. Umahuluti huu unahusu mwingiliano wa sifa za usimulizi na uandishi ili kuunda utanzu huu tofauti na mtazamo wa hapo awali.

Ili kutekeleza lengo letu, tumetumia machapisho matatu ya hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Tumechagua hadithi tatu kwa kila chapisho ili kuweza kupata data ya kutosha kuhusu utafiti wetu. *Pendo la Heba* (1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Kutokana na utafiti huu umahuluti wa hadithi fupi unaweza kuchanganuliwa kwa kutumia vigezo vya nadharia ya mwingiliano matini. Mwingiliano huu unahusu mwingiliano kati ya sifa za usimulizi na sifa za uandishi katika hadithi fupi za kisasa. Mwingiliano matini ni nadharia inayohusu kuchangiana na kuingiliana kwa sifa mbili au zaidi. Nadharia hii inasisitiza kuwepo kwa matini ya hapo awali itakayoadhiri matini ya sasa hivi na hata itakayotungwa baadaye.

Nadharia hii imetusaidia kuhusisha mwingiliano wa sifa za usimulizi na uandishi katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Imeweza kutusaidia kuhusisha matini ya awali, ambayo husababisha matini ya sasa na matini itakayojiri baadaye.

Imebainika kuwa katika *Pendo la Heba* (1997) sifa kadhaa zimejitokeza. Mazungumzo ni sifa ambayo imetumiwa sana na waandishi wa makala hasa ya fasihi. Mazungumzo hata hivyo hayapatikani tu katika usimulizi, jinsi tulivyoyajadili yamepatikana katika uandishi kusisitiza maudhui ya mwandishi. Wahusika wanapozungumza katika uandishi, wao huweka wazi hisia zao wenyewe, hutoa maoni yao, misimamo yao na kwa kufanya hivyo huibua maudhui zaidi.

Mazungumzo, yalitumiwa ili kuweka wazi hisia za wahusika. Maelezo ya aya, yanayoelezea matukio kwa ufupi, ili kumweleza msomaji kufahamu vyema ujumbe wa mwandishi. Mazungumzo yalitumiwa katika *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. (2000) pamoja na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Mazungumzo yametumiwa baina ya wahusika wawili au zaidi katika uandishi na hata usimulizi.

Katika mazungumzo, kukatiza sentensi ni sifa iliyojitokeza mara nyingi. Mara kwa mara mzungumzaji atakatiza mazungumzo ili kutafuta neno mwafaka la kutumia. Katika hali ya kutafuta neno hilo mzungumzaji atajikuta akirudiarudia neno ili kupata neno mwafaka. Mazungumzo ni sifa nyingine tuliyoichunguza katika sura ya tatu kama mojawapo wa sifa za usimulizi na vilevile hujitokeza katika uandishi.

Matumizi ya methali na nyimbo ni sifa zingine tulizozishughulikia. Sifa hizi za usimulizi zimetumiwa katika uandishi kuweka wazi maudhui ya mwandishi na hata msimulizi. Nyimbo zimetumiwa kuwatumbuiza wasomaji na wasikilizaji katika hadithi fupi za kisasa. Kulingana na utafiti wetu, nyimbo siyo tu sifa ya usimulizi ya kuyaweka maudhui ya msimulizi wazi, bali pia ni sifa inayorutubisha uandishi. Nyimbo zilitumika katika baadhi ya hadithi tulizoteua ili kupunguza machovu ya maelezo mengi ya mwandishi. Nyimbo hizi pia zilitumika kuisisitiza zaidi ujumbe wa mwandishi kwa wasomaji.

Monolojia ni sifa ambayo ilitumiwa ili jinsi wahusika wanavyozungumza na nafsi zao. Kuzungumza huku, kulionyesha matamano, machungu ya wahusika. Monolojia huweka wazi mawazo ya ndani ya wahusika katika uandishi na hata mawazo ya ndani ya msimulizi ili kuifanya hadhira ifikiri kwa undani kuhusu ujumbe unaoenezwa na msimulizi. Sifa hii ya Uradidi ni sifa ambayo tumeitazama. Uradidi ulitumiwa katika hadithi hizi, ili kuisisitiza dhana muhimu. Uradidi ulitumiwa ili kumfanya msikilizaji kukumbuka yale yaliyosimuliwa. Katikakuisisitiza jambo fulani, mwandishi au msimulizi huweza kuyaweka wazi matamano yake kuhusu ujumbe wake kwa wasomaji au wasikilizaji.

Sifa ambazo tulizichunguza katika sura ya nne zilikuwa sifa za uandishi ambazo pia ziliibuka katika usimulizi. Tuliona kwamba maelezo yalimpa fursa mwandishi kueleza kuhusu mhusika na hali yake. Msimulizi naye anaweza kueleza matukio fulani kuhusu karamu ya wanyama anaowasimulia katika hadithi yake. Anaweza kutoa maelezo kuhusu safari ya wanyama na jinsi walivyovalia katika karamu fulani. Msimulizi anayeitamba hadithi atayatumia maelezo ya moja kwa moja ili kufafanua ujumbe wake. Kuzingatia tasnifu yetu, sifa ya maelezo haijitokezi tu katika uandishi pia hutumika katika usimulizi.

Sifa nyingine ya uandishi na hata usimulizi ni upenyezi wa mwandishi mwenyewe katika hadithi au kisa anachokisimulia. Mwandishi hutoa maoni yake kuhusu wahusika, tabia yao katika mtiririko wa hadithi. Mwandishi hutathmini mielekeo yao, hali ya maisha na hata kupendekeza mienendo yao. Hali hii hujitokeza katika usimulizi ambapo msimulizi hutathmini wahusika fulani kulingana na matendo yao. Sifa ya mwisho tuliyoijadili ilikuwa matumizi ya barua. Barua ni sifa nyingine ambayo imetumiwa. Katika hadithi, uzungumzi nafsi umetumiwa sambamba na barua ili kuzua hisia za ndani za kirafiki. Barua zilitumika katika ili kuisisitiza hoja za mwandishi kuhusu maudhui yake na kuyaweka wazi.

Sifa hizi tulizozitaja hapo awali hutumiwa katika masimulizi na katika uandishi huku zikichangiana katika usimulizi au andishi. Madai kuwa hadithi fupi, ni mwendelezo wa kiistari ya ngano huenda hayana mashiko kabisa. Umahuluti unajitokeza katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Kutokana na matokeo ya utafiti wetu tulibaini kuwa sifa hizi za usimulizi na uandishi huenda sambamba katika maandishi ili kukamilisha maudhui ya mwandishi.

Sifa hizi hutumika kwa pamoja katika usimulizi na hata uandishi .Katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili sifa hizi huingiliana ili kuunda utanzu huu ambao ni mahuluti. Utanzu huu mahuluti unadhihirisha mwingiliano wa sifa hizi ili uwasilishe ujumbe wa mwandishi. Utanzu huu wa hadithi fupi ya kisasa,ni mwingiliano wa sifa za usimulizi na uandishi.

5.2 MCHANGO

Kazi hii imetoa mchango kwa uchanganuzi wa hadithi fupi za kisasa za Kiswahili.Imechangia kwa kubainisha mtazamo tofauti wa kuutazama uatanzu huu wa hadithi fupi ya Kiswahili.Utafiti huu pia umetumia nadharia ya mwingiliano matini katika kuchunguza umahuluti katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili.Nadharia hii inaweza kutumika katika kuchanganua tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili.

5.3 MAPENDEKEZO

Kulingana na utafiti wetu tulionyesha kuwa nadharia ya mwingiliano unaweza kutumiwa katika kuelezea umahuluti katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Hata hivyo utafiti wetu hautoshelezi kutoa maelezo yote juu ya umahulutu. Utafiti huu hautoshelezi kwa sababu ya muda ambao ni mfupi na mambo ni mengi ya kushughulikia. Mapendekezo yetu ni kuwa utafiti zaidi ufanywe ili kufafanua na kuendeleza zaidi swala la umahuluti katika hadithi fupi.

Miruka (1994) anasema kuwa katika uwanja wa fasihi utafiti umefanywa juu ya mtindo, maudhui na utendakazi wa matini. Utafiti huu ulijikita katika kuchanganua zote kwa pamoja. Mapendekezo yetu ni kuwa mengi yatafitiwe jinsi sifa za usimulizi na uandishi zinavyowasilisha maudhui ya hadithi fupi huku sifa hizi zikihusiana.

Utafiti mwingine unaweza kufanywa zaidi kuhusu nadharia hii na vipengele vyake kutumiwa kwa kuchanganua hadithi fupi za mwanzo. Utafiti zaidi unahitajika kufanywa kuhusu wahusika na jinsi walivyochorwa katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili. Sifa zingine za usimulizi na uandishi, zinaweza kuangaliwa kwa upana zaidi, katika hadithi fupi za sasa za Kiswahili.

Katika utafiti tulikumbana na matatizo kama vile uchache wa kazi zilizohakikiwa katika uwanja wa utanzu huu wa hadithi fupi, kuhusisha nadharia na mada tuliyoitcua na mwisho kutofautisha sifa hizi za usimulizi na uandishi kwa uwazi.

MAREJELEO

- Allen, G. (2000). *Intertextuality*: New York. Routledge 29 West 35th Street.
- Bailey, T. (2000). *On writing short stories*. New York: Oxford University Press.
- Bakhtin M. (1981). *Theory of the Text*. London: Routledge.
- _____ (1986). *Speech Genres and other late Essays*. London. Harvard University Press.
- Banzi, A. (1980). *Tamaa mbele na Hadithi Nyingine*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
- _____ (1982). *Nipe Nikupe na Hadithi Nyingine*. Ndanda-Paramiho. Benective Publications.
- Barshad Y. (1980). *Dhuluma na Hadithi Nyingine*. Dar es Salaam. Busara Publications.
- Finnegan R.(1970) *Oral literature in Africa* London: Oxford University Press.
- Forster,E.M.(1927) *Aspects Of The Novel*;London: Penguin Books.
- Gibbe A. G. na T.A. Mvungi (1987) (Wahariri] *Fasihi simulizi kwa sekondari na vyuo*. Dar es Salaam. Standard Publishing Company.
- Grand Saigne, J.(1985) (Mhariri) *African Short Stories*; Nairobi: Macmillan Press
- Haggard R. (1935) *Hekaya za Abunuwazi*.London: Macmillan Press.
- Harris R. (1986) *The Origin of Writing*. London: Maccmillan Press

- Kinge'i G.K. na
R.M. Wafula (1997) *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine.*
Nairobi.Chama Cha Waandishi.Kenya.
- Larson L. (1978) *Oral Features in Written: The emergence of
African fiction.* London;Macmillan Press
Ltd.
- Lord A. B. (2000) *The singer of tales.* London;Harvard
University Press.
- Mbatiah M. (2000)
(Mhariri) *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*
Nairobi;Jomo Kenyatta Foundations
- Mbele J. L. (1982) *Oral literature and the Writing Tradition.*
Kiswahili Toleo 49/1. Dar es Salaam;TUKI
- Miruka O.(1994). *Encounter with oral literature.* Nairobi;
East African Publishers
- Mohamed S.A (1978). *Si Wazimu Si Shetani .* Nairobi;Longman.
- _____ (1995) *Kunga za nathari ya Kiswahili. Tamthilia,
Riwaya na Hadithi Fupi.* Nairobi;East
African Education Publishers
- Mohammed M.S.(1976) *Nyota ya Rehema:* Nairobi;
Oxford University Press African
Educational Publishers.
- _____ (1978). *Kicheko cha Ushindi.* Nairobi;Shungwaya
Publishers.
- Mohochi, E.S. (1995). *Fani katika Hadithi Fupi.* Tasnifu ya
Uzamili;Chuo Kikuu cha Egerton.
- _____ (1997). *Hadithi fupi utanzu uliopuuzwa. Mulika
Nambari 24.* Dar es Salaam;TUKI
uk. 63-68

- _____ (2000). *Fasihi ya Kiswahili katika karme ya21: nafasi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam;TUKI.
- Mphahlele,E (1996). *A guide to Creative Writing.* Nairobi;East African Literature Bureau.
- Msokile M. (1981). *Nitakuja kwa Siri.* Dar es Salaam;Dar es Salaam University Press.
- _____ (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Dar es Salaam; Educational Publishers.
- Muriithi J.J. (2002) *Usemezano Katika Tamthilia ya Kiswahili.Tasnifu ya Uzamili;* Chuo Kikuu cha Kenyatta
- Mwanzi, H. (1987). *Notes on Chameleons Second Delivery.* Nairobi: Heinemann Publishers.
- _____ (1995). *The style of the short story in Kenya. An analysis of the short stories of Ngugi wa Thiong'o, Leonard Kibera and Grace Ogot.* Ph.D University of Nairobi.
- Ngure A. (2003) *Fasihi simulizi; kwa shule Za Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers
- Njogu k. (1997) *Uhakiki wa Riwaya za visiwani.* Nairobi: Nairobi University press.
- Ong W. J. (1982) *Orality and Literacy: The Technologizing of the Wor;* London Methuen.
- Parker D. (1965). *Short Story: A thematic Antology.* New York. Charles Scrubner Sons Publishers.
- Poe E.A. (1938) *The complete Tales and Poems.*New York: Random Housen Inc.

- Robert S. (1951) *Kusadikika*. Nairobi Nelson & Sons Ltd.
- _____ (1968) *Siku ya Watenzi Wote*.
Nairobi; Nelson & Sons Ltd
- _____ 1968) *Kufikirika*. Nairobi: Oxford University Press.
- Ruhumbika G.(1974) *Parapanda na hadithi nyingine*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.
- _____ (1978). *Uwike Usiweke kutakucha*. Arusha: East African Publishers.
- Schwiebert J. E. (2001) *Reading and writing from literature*. Boston U.S.A Houghton Mifflin Company.
- Sengo, T.Y. (1982). *Fasihi* . Dar es Salaam: Nyanza Publications Agency.
- Senkoro, F.E.M.(1982) *Fasihi*. Dar es salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Senkoro, F.E.M. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Publicity Centre.
- _____ (1989). *Jamila mpenzi na Hadithi Nyingine*. Dar es Salaam: Publicity Centre:
- Steere E. (1989) *Swahili Tales as told by the natives of Zanzibar*.
- Wamitila K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- _____ (2003). *Kichocheo cha Fasihi. Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.
- _____ (2004)
(Mhariri) *Mayai waziri wa Maradhi na hadithi nyingine*. Nairobi: Focus Publishers.